# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

Verbatim Report Of

# DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL – KILGORIS CONSTITUENCY HELD AT KILGORIS COUNTY HALL

ON

16th OCTOBER, 2002.

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, KILGORIS CONSTITUENCY HELD AT KILGORIS COUNTY HALL ON 16TH OCTOBER, 2002.**

**Secretariat in Attendance:**

1. Mr. George Nakholi - Programme Officer
2. Maurice Kepoi Raria - Assistant Programme Officer

The meeting started at 11.00AM with Maurice Kepoi Raria – Programme Officer in chair.

**Raria:** Mnaweza kutoa maoni yenu ama kama kuna mambo yoyote ambayo hayakuwa wazi ambayo hamkuelewa basi itakuwa ni furaha yetu kusikia maoni yenu na pia maswali yoyote na tutajaribu kujibu tuwezavyo, asanteni.

**Prayers**: Asante sana. (inaudible) *Rabbana takabal minna wal Alhamdullillahi Rabil Alamin – AMIN.*

**Philip T. Saiyuah:** Hawa wenzetu kutoka Nairobi wamekuja kututembelea na kama tunavyojua wamekuja kwa sababu ya kazi yetu ya Marekebisho ya Katiba. Hapo mbeleni tumekuwa na ma-Commissioners wengine mara mbili wamekuja, wamewahi kuja hapa, walikuja kwa civic education mpaka wakati waliporudi hapa tena kuchukua maoni yenu. Vile mlivyotoa maoni tulisema kwamba maoni itaenda Nairobi iandikishwe … halafu itarudishwa hapa kwenu drafts mbili, yetu hapa vile tulivyosema na tuanze ku-discuss. Kwa hivyo siku ya leo tuko hapa tunataka kuanzisha mafundisho ya Katiba mpya.

Kwa hivyo nitawajulisha wageni, Mr. Raria who is a Programme Officer, Mr. Nakholi who is also a Programme Officer from our head office. Kwa hivyo, sasa ningelipenda kama kuna delegate members wako hapa wale waliendesha hii kazi wasimame nipate kuwajulisha na the 3Cs members, ikiwa wamefika wasimame ili nipate kuwa-introduce, sema jina Bwana Keiyo na una-represent constituency gani?

**Bwana Keiyo**: (inaudible)

**Nakholi:** Asante sana District Co-ordinator, yangu ……. (inaudible), wazee wote kutoka Trans Mara District, mabibi na mabwana nawasalimu nyote hamjambo?

**Audience**: Hajutambo.

**Nakholi:** Hamjambo tena?

**Audience**: Hatujambo.

**Nakholi:** Basi tumekuja kuangalia yale ………..(inaudible). Nataka tu kuomba radhi kuna Commissioner ambaye alikuwa na sisi ambaye ni Bwana Keriako Tobiko hangeweza kuwa na sisi kwa sababu hakuwa anasikia vizuri sana, hata jana tulikuwa (inaudible)…. lakini hakuweza kufika sababu ya afya. Kwa hivyo ile kazi tutafanya leo, tutafanya kwa niaba yake na tukiifanya mjue ya kwamba hii kazi ni ya Commission na itafika huko.

Jambo muhimu tumekuja hapa kufanya ni kuchambua yale maneno mlitoa, vile mlikuwa mnatoa maoni yenu na muone ya kwamba yako hapa au kuna tofauti na ikiwa kuna jambo lolote pia mnaweza kutoa tutaandika chini ….(inaudible). Yule ambaye ana jambo lolote ambalo anaweza kufikiria baadaye kama tukishaondoka, anaweza kuandika kama umeshaangalia hii pull-out sasa na unaona jambo ambalo unataka kuongeza, kama haujatoa mawazo yako uandike na upatie District Co-ordinator alete kabla ya tarehe ishirini na tatu. Commission itakaa tarehe ishirini na nne na itaangalia mambo yote kutoka kwa constituencies zote mia mbili na kumi, Trans Mara ikiwa moja yao.

Kwa hivyo (inaudible)…. ya kwamba ………..kutoka kwa District hii ya Trans Mara na kama mumeangalia Nation ya leo utaangalia page ya Rift Valley utaona lile taangazo la wale walichaguliwa kutoka hapa kama mnaweza kuwajua kutoka Rift Valley na Trans Mara mjue delegates watakuja kwa Conference hii.

**Raria:** (inaudible)

**Nakholi**: Sasa mmesikia hawa watu watatu ndio wamechaguliwa na wamekuwa gazetted kama delegates kutoka District hii ambayo ni one constituency District. Kwa hivyo, sijui kama mmoja wao ako hapa au watatu au wawili wako hapa, hakuna shida nilitaka tu kama wako hapa wasimame tuwaone lakini nafikiri mmewaona hapo mbeleni.

Vile mmeona tungeanza mkutano huu saa nne lakini sisi tulikuwa hapa kama saa tatu na …..(inaudible) lakini tuliambiwa korti inafanyika hapa na tutapewa nafasi baadaye ……… wanajua tumechelewa kidogo. Kwa hivyo, sina jambo lolote tutaendelea na kazi na ……. Bwana Raria ni mmoja wenu aanze na lile jambo ambalo …..(inaudible)

**Raria:** Asante sana Bwana Nakholi, the District Co-ordinator na watu wa sehemu ya Trans-Mara ambao wamekuja katika hiki kikao. Hata sisi tumefurahi kuwa nanyi siku ya leo, kwangu ni mara ya kwanza kuja hapa (inaudible). Jumapili iliyopita nakala hizo zilikuwa zimechapishwa kwa gazeti ya Taifa Leo na nafikiri wale hawajawahi kuangalia hiyo gazeti nakili ya Kiswahili ilikuwa mle ndani kwa hivyo, kama unaweza kupata gazeti ya jumapili iliyopita basi tutapata nakala ya Kiswahili.

Basi ningependelea sana kuanza kueleza hasa kwa ufupi Katiba ni nini na ningependelea kuwaambia ya kwamba, Katiba ni mkataba wa masikizano baina ya wananchi, baina ya watu wanaoishi katika sehemu moja wanaoita nchi yao. Hivyo basi, Katiba inatokana na watu wa nchi ama sehemu fulani kuketi pamoja halafu wanajadiliana mipango fulani ambazo zitawasaidia kuweza kutekeleza mambo yao ya kila siku.

**Philip T. Saiyuah**: Bwana DC kama unavyojua kwamba tulikueleza kwamba leo tutakuwa na kikao hapa na wenzangu na isipokuwa tumeanza karibu tumechelewa kidogo lakini ninaweza kukujulisha wenzangu hapa. Huyu ni Ole Raria, Mr. Nakholi both of them are Programme Officers na this is our DC Fred Musami.

**Raria:** Asante sana Bwana District Co-ordinator na Bwana DC. Nilikuwa nimeanzisha kupitisha wananchi nilikuwa nimeanza kuwaeleza hasa Katiba ni kitu gani na nilikuwa nimeanza na kusema ya kwamba Katiba ni mkataba wa masikizano baina ya watu wanaoishi sehemu moja ambayo wanaita nchi yao na ukiangalia katika Katiba vile ilivyo hivi sasa, wananchi walikuwa wameweza kutoa maoni yao mengi. Wananchi walikuwa wametoa shida zao nyingi sana lakini haingewezekana shida hizo zote ambazo walisema ziweze kunakiliwa katika Katiba, kwa sababu Katiba hasa ni kama ramani, ni kama road map ya kuonyesha wananchi njia watakayopita. Na ukiangalia ramani ama ukiangalia road map haiwezi kukuonyesha mahali kuna shimo katika njia, haiwezi kukuonyesha mahali kuna milima katika hiyo njia ama mahali kuna pot holes, bali road map inakuonyesha kwa ujumla upande ambao utapita na hivyo hasa ndiyo Katiba inavyoundwa. Katiba inaguzia sehemu tofauti ambazo ni za muhimu katika taifa kama vile utawala, hali ya sheria na mambo mengine kama hayo.

Ninaweza kuwaelezea kwa kifupi sana kwamba historia ya Katiba tuliyo nayo hivi sasa, Katiba tuliyo nayo iko na miaka thelathini na tisa na kati ya hizo miaka thelathini na tisa Katiba ya Kenya imewahi kubadilishwa mara thelathini. Nikijaribu kufananisha na Katiba ambayo ni kongwe sana ya nchi ya Marekani ambayo iko na miaka mia mbili, imewahi tu kubadilishwa mara ishirini pekee yake. Nataka uangalie mfano huo ambayo Katiba ya Marekani iliyo na miaka mia mbili imebadilishwa mara ishirini pekee yake na Katiba ya Kenya yenye miaka thelathini na tisa na imewahi kubadilishwa mara thelathini ikimaanisha ya kwamba basi kuna kasoro katika Katiba tuliyo nayo kwa sababu ikiwa inabadilishwa mara nyingi namna hiyo basi yaonyesha hata msingi wa kubuniwa kwa Katiba hiyo ulikuwa na kasoro, na ndiyo sababu wananchi waliweza kupata msisimko mkubwa sana wakaitisha katika nyadhfa mbali mbali kwamba, ni vyema nchi hii kupata Katiba mpya ambayo inamulika mahitaji yao ya wakati wa sasa.

Kwa sababu Katiba ambayo ni mzuri ni ile ambayo inamulika mahitaji ya watu ikitumia lugha ya wakati ulioko. Kwa hivyo, Katiba inapaswa kunakili shida za wananchi na ni Katiba ambayo inaweza kutumiwa kwa vizazi na vizazi. Hivyo basi ndiyo Tume iliweza kubuniwa ya kubadilisha Katiba na wakaja wakaweza kubuni Katiba ambayo mko nayo hivi sasa na mkiangalia tofauti kubwa sana kati ya Katiba ya sasa na hii Katiba mpya ni kwamba Katiba hii ya sasa iko na utangulizi na kwa hiyo nakala inaitwa Preamble. Kwa hivyo, mkiangalia hapo mwanzo mwanzo kabisa, mtaona kwamba Katiba mpya iko na utangulizi.

Wananchi walisema ya kwamba ni vyema hasa Katiba yetu iwe na utangulizi kwa sababu utangulizi unamulika mambo muhimu sana ambayo yanashikilia taifa na ukiangalia utangulizi wa Katiba mpya unajaribu kueleza Wakenya ni kina nani kwa sababu Katiba tuliyo nayo hivi sasa imetenga watu wa Kenya na haiwatambui kabisa. Lakini Katiba mpya inaeleza wazi wazi ya kwamba, 'sisi wananchi wa Kenya' na inazidi kufafanua ya kwamba 'tukifahamu wingi na tofauti zetu za kikabila, kitamaduni na kidini na tukidhamiria kuishi kwa amani na umoja kama taifa moja huru lisilogawika', kwamba Kenya ni taifa na Wakenya wako na tofauti kulingana na kabila, kulingana na utamaduni na pia wako na tofauti ya hisia za kidini. Lakini zaidi ya hayo yote, licha ya tofauti hizo, Wakenya wanadhamiria kuishi wote pamoja kwa amani katika nchi yao moja isiyogawika.

Kwa hivyo, mkijaribu kuzingatia hasa maneno mafupi sana ambayo yamenakiliwa katika utangulizi, yanajaribu kutupatia picha ya Katiba mzima. Yale maneno machache ambayo yamewekwa katika utangulizi yanasimamia mambo yote ambayo yamezungumziwa katika Katiba hii mpya. Ukisoma Katiba kwa undani, kuna maneno ambayo Katiba hii imezungumzia ama kupatia uzito, Katiba hii imezungumzia juu ya umoja wa kitaifa, imezungumzia juu ya kutambua kwa utamaduni wa kila mtu, Katiba hii pia imezungumzia juu ya demokrasia na uwajibikaji. Imezungumzia pia, kuheshimu watu wote bila ubaguzi wa sehemu yoyote ya taifa, Katiba hii pia imeweka uzito hasa mambo ya kuangamiza ufisadi, imezungumzia pia kuwajibisha wote katika maendeleo.

Katiba pia imezungumzia mambo ya uongozi bora, ugawaji sawa wa rasilmali, udumishaji wa sheria, haki za kimsingi na maslahi ya watu wanaoishi katika jamii kama vile walemavu na kina mama. Kwa hivyo, ukiangalia Katiba hii imezungumzia hasa mambo kama hayo vile tutakavyoona kwa muda mfupi, na tunasema kwamba je, madaraka ya Katiba iko namna gani? Mkiangalia kwa hizo nakala zenu mtakuta mahali ambapo inasema au iko na kichwa cha Supremacy of the Constitution ama ukuu wa Katiba. Na tunasema ya kwamba Katiba ni sheria kuu ya msingi na hivyo basi kama ni sheria kuu ya kimsingi basi mfumo wote wa serikali, sheria nyingine yoyote ama mtu yoyote katika nchi, basi ni lazima awe chini ya Katiba.

Kwa hivyo, tunasema kama Katiba ni kuu, basi Bunge liko chini ya Katiba, Rais wa nchi ako chini ya Katiba na maofisi zote za serikali kwa sababu zimebuniwa kutokana na Katiba, ofisi zote za uma ziko chini ya Katiba. Hivyo basi, tunasema ya kwamba jambo muhimu katika Katiba hii inaonyesha vizuri sana ugawaji wa mamlaka ambayo tutaona hivi sasa na ningependelea tu kuwapatia muktasari huo ili tukienda kutoka ukurasa moja hadi mwingine, tuwe pamoja. Kwa hivyo, kwa mambo ya muktasari juu ya Katiba na juu ya utangulizi ningependa kufika hapo ili tuende katika sehemu muhimu ambazo hasa zinahusu sehemu hii. Tunajua sehemu za Kajiado, sehemu za Narok wameongea sana juu ya mambo ya ardhi na tungependelea kuanzia katika hizo kurasa ambazo watu wa sehemu hii walitilia mkazo. Kwa hivyo, kama hakuna swali lolote tungeenda kuanzia mambo ya ardhi lakini kama kuna mtu ana swali lolote kuhusu Katiba vile nimesema kwa muktasari ama kama uko na jambo lolote ungependa kuzungumzia juu ya utangulizi basi huu ni wakati wako, asante.

**Philemon**: Ninaitwa Philemon na ninatoka katika youth wing inaitwa *Matonyo*. Jambo ambalo ningependa tu kuongeza

kidogo ni ya kwamba tulipotoa maoni inaonekana Tume iliweza kuangalia juu ya Preamble na tunashukuru sana sababu mumeweza kutambua wananchi wote na mkayafanya hayo yawe ya manufaa zaidi. Jambo lingine ningetaka tu kuongezea ni tunaombea kwamba hiyo Preamble iweze kuwa ni hiyo tu na isibadilishwe sababu tunasikia kwamba wataenda National Conference na sijui kama ningependa tu ya kwamba muweze kuchunguza kupatiana maoni ili wananchi wote waweze kutambua sababu mumetambua maoni ya wananchi. Ni hayo tu nilikuwa nikisema ili tuweze kuangalia mambo mengine yaliyoko mbele yetu.

**Nakholi:** Kabla sijaenda mbele labda ningeguzia tu ya kwamba, kuna hii interim report ambayo mlitoa maoni yenu na tumerudisha hapa na kwa wakati ule unaofaa mnaweza kutembelea District Co-ordinator kwa ofisi yake muangalie yale mambo ambayo mlichangia wakati ule. Sasa tunayarudia na kitabu kiko hapa ambayo ni report ile mlifanya mkatoa baadaye na hii ndiyo interim report, asante sana kwa kuchangia kwa hiyo Preamble.

**Gedion Ole Nyoto:** Jina langu ni Gedion Ole Nyoto Chief Mkuu kutoka Trans-Mara. Kwanza nashukuru kwa nafasi hii ambayo mumetupatia wale ma-Commissioners ambao wako hapa na wageni wengine na wananchi wenzangu kupata nafasi hii pia ya kusema jambo moja hata ingawa hatujaendelea zaidi kwa sababu tulitaka kuchangia baada ya kuelewa hii proposal yote ndiyo tutapata yale ambayo tutaweza kuchangia. Lakini kile ambacho kimenifanya nikuje hapa mapema hivi ni vile mliguzia ya kwamba Katiba yetu bado ni changa sana ikilinganishwa na zile za nchi zingine hasa ile kongwe ya Katiba ya nchi ya Marekani ya kwamba iko na miaka mia mbili na imewahi kubadilishwa tu mara ishirini na tisa na yetu ina miaka thelathini na kitu na imebadilishwa mara thelathini.

Hii inaonyesha kwamba pengine huwa tunafanya kasoro fulani fulani kabla hatuja-settle ya kwamba sasa hii iwe Katiba yetu kwa sababu ni lazima kuna loop-hole ambayo imeonekana ndiyo tumefanya au Katiba imewahi kubadilishwa mara mingi hivi. Na kile ambacho tungeomba kwa wakati huu tena ni kwamba kwa sababu hii ni nia ya wananchi na ni matakwa ya wananchi kutaka Katiba mpya ambayo itaongoza at least muda ambao kutakuwa na nafasi ya kuongoza Kenya hata miaka hamsini au na kama zile zingine.

Tunasema kwa wakati huu pia tusije tukarudia kile ambacho kimetufanya turudie Katiba mara mingi na ndiyo tunaomba ya kwamba Katiba hii ipatiwe muda wa kutosha na wananchi wapate kuchangia ya kutosha mpaka wakati tutakapokwenda kutoa the final draft, iwe basi itaweza kutuongoza kwa muda mrefu zaidi kuliko kuibadilisha kila mara tukijua ya kwamba itahitaji rasilmali ya Wakenya na tutakuwa tukiweka pesa nyingi mahali pamoja, ile pesa ambayo tungefanyia miradi mingine ya maendeleo. So tunaomba ya kwamba kwa wakati huu tena tusije tukafanya makosa au tukatoa mianya ambayo itaweza kuturudisha hapa mwaka baada mwaka au baada ya mwaka mbili tuko hapa tena lakini tuangalie sana na hivyo tunaomba muda zaidi upatiwe hii kazi ili tuje na final draft.

**Nakholi**: Hayo ni maoni tumeyachukua na wakienda Conference, hilo ndilo jambo moja watakuwa wanaangalia kama na ile

request umefanya ni maoni umetoa imeingia na Commission iangalie.

**Johana Ng'eno Kipyegon:** Asante sana waheshimiwa Commissioners na Co-ordinator. Kwa majina ninaitwa Johana Ng' eno Kipyegon ninaishi hapa Trans-Mara, na kwanza kabisa waheshimiwa ni kwamba ningependelea kabla sijaguzia kidogo yenye iko hapa, kuomba wananchi wenzangu tuungane pamoja kupinga ile hatua ya ma-Jaji wawili kupeleka kesi kortini kukatalia hii maneno ya Constitution yaangaliwe hapa Kenya. Kwa hivyo tunawaomba kwa sababu tumetumia pesa mingi muda mwingi na bado tunaendelea kukaa hapa na kuna watu wachache ambao hawajaridhika, tungependa haswa sana sisi wananchi tuungane kwa sababu hii ni kitu yetu, hii ni future yetu, hii ni mali yetu, kwa hivyo tupinge sisi sote hii kazi iendelee.

Jambo la pili ni kuhusu ma-representatives ambao walichaguliwa hapa Trans Mara kuwasilisha ama kuenda kwa huo mkutano wa kujadili hii constitution. Well sijui sana ni criteria gani ilitumika waheshimwia lakini ningependa kusema ya kwamba, haswa uchaguzi uliofanywa haukufanywa kwa njia safi na wale wawakilishi waliotolewa ningependa tu kukueleza ya kwamba huenda ikawa ni ya kuwasilisha matakwa ama vitu vya mtu mmoja sio vya watu wote wa Trans Mara. Kwa sababu hapa Trans Mara tuko na communities ambao, you know when actually this idea was proposed, ilisemekana ya kwamba lazima tukuwe na one gender ama one woman ambaye lazima awasilishe naye pia ama who will represent kwa niaba ya wakina mama wote wa Trans Mara. Na kwa hivyo, mama mmoja alitolewa yes there is no problem, but the problem is, pia hii constitution ikiletwa inafaa kuwahudumia ama kuangalia maslahi ya wa-Trans Mara wote kwa ujumla lakini ukiangalia imewasilisha anga one community because not all the communities have been represented in that particular issue na hii constitution ikikuja hapa Trans Mara lazima ihudumie all the communities who are in Trans Mara. Kwa hivyo, ningependelea if there is to be any review or if there shall not be, it has to be taken in that not all the people are represented in Trans Mara in that Review.

Jambo la tatu ni kuhusu Land. Well, concerning the Preamble of this Nation, tumefurahia na tunakushuru sana kwa kile kitu ambacho mliandika kama Preamble ya wananchi. Hiyo preamble inaonyesha ya kwamba matakwa ya kila mwananchi yatatekelezwa, the gender issue, ethnicity, the political affiliation, the problems facing the wananchi imeguzwa na tungependa kushukuru sana na hiyo preamble ikae hivyo na kama kuna kuongeza kidogo iongezwe kidogo lakini it has to be like that. Otherwise, thank you very much.

**Raria:** Kwa kusema kweli shida ya wale wanaokwenda kuwakilisha constituency katika National Conference, hii shida pia tulipata katika sehemu ya Narok South na ningependa kuwahakikishia ya kwamba ni jambo ambalo tutatilia mkazo sana kwa sababu ilikuwa ni nia ya Katiba kuhakikisha ya kwamba wananchi wote wanawakilishwa kwa usawa na ndiyo sababu walitoa mbinu fulani za kuhakikisha ya kwamba watu wote katika kila wilaya ikiwepo kina mama na pia kujumuisha jamii zote zilizo katika kila wilaya kwa sababu ni hivyo tu ndiyo tutaweza kupata uwakilishi wa haki.

Kwa hivyo, hiyo shida tulisikia na ilitiliwa sana mkazo kule Narok South na ningependa kuwahakikishia kuwa hilo jambo tutapeleka katika Commission na kabla ya muda mrefu mtapata reporti. Na pia kama District Co-ordinator anaweza guzia

jambo hilo la jinsi representatives walivyochaguliwa kama ana maoni yoyote angetaka kutoa kwa wakati huu basi ni nafasi nzuri anaweza pia kutueleza.

**Philip T. Saiyuah:** Asante sana Bwana Ng'eno kwa kuguzia vile hawa wenzetu watatu walipochaguliwa. Criteria tuliyofuata hapa ni criteria yenye tulipatiwa kutoka Nairobi head office kwamba wale watu wenye wako interested kuenda Nairobi wafanye application tulitangazia watu wakakuja wakafanya application, halafu head office yetu ikaweka siku ya kufanya uchaguzi. Na wale watu ambao wangechagua hawa watu ni Councillors, Commission ilikuja ikajadiliana huko juu ikakuja ikafikia kwamba Councillors katika kila district watakuwa Electoral college na tarehe kumi na saba tuliitana hapa. Councillors wa Trans Mara walikuja tukawapa majina ya wale applicants. Wao wenyewe wakafanya uchaguzi hapa bila maneno yoyote, wakatupatia hawa wananchi watatu, Dr. Mbilei, Councillor Imado na Tecla Munguch.

Siku hiyo tulifanya uchaguzi wa amani kabisa hakuna mtu yoyote alisema tulifanya kwa njia mbaya au community hii na ile haikuwa represented. Kwamba watu wa Kipsigis kulikuwa na applicants kama wawili hivi, mmoja akapata kura mbili na wale tuliwachagua ni wale walishinda, hatukutumia njia ingine ya kinyume.

**Nakholi:** Asante sana.

**Olenga Mining:** Jina langu ni Olenga Mining. Nafikiri mimi pia niko na maoni tofauti kwa sababu jamhuri yetu ya Kenya ni nchi ambayo ni ya vyama vingi vya kisiasa na commission hii ilikubalia Local Authorities kuwa ndiyo wana mamlaka ya kuchagua. Hii ni kusema ya kwamba basi Katiba hii haitakuwa na maana, haitakuwa ni Katiba ya wananchi kwa sababu wananchi ndio wangepewa nafasi ya kuchaguwa wale representatives ambao watakwenda kuwakilisha hao katika National Conference.
Kwa hivyo, maoni yangu ni ya kwamba ingefaa commission iruhusu at least watu wengine wanne katika Trans Mara ambao watakuwa wana-represent hizo communities nne, hawa watatu ambao wamechaguliwa wakiwa pamoja wawe watu saba, thank you.

**Raria**: Bwana Daniel tumesikia mawazo yako na tutahakikisha ya kwamba hii shida ya representation ambayo tumesikia sasa kwa constituency mbili na imetiliwa mkazo sana na tuliona uchungu mwingi sana jana upande wa Narok South na hata hapa inaonekana hiyo pia ni shida, tungependa kuwahakikishia mara ya pili ya kwamba hiyo shida lazima tupeleke head office ama kwa kweli hiyo ndiyo shughuli ambayo wametutuma kufanya hapa, kuja kusikiza maoni ya wananchi. Kwa hivyo, tusipo-report jambo kama hilo ambalo linawakera sana, basi hatutakuwa tunafanya kazi yetu.

**Kalasinga**: Mimi ni Kalasinga na ninafanya na Administration na kwa upande huo wa representation, mimi nimeamuka kwa sababu nimesikia yule area representative wa hii Constitution Review Commission ametuelezea ile criteria ambayo imetumwa kutoka Nairobi itumiwe hapa. Na mimi sina shaka kwamba sisi tumeletewa jambo hapa kutoka Nairobi na ikifika hapa ofisi

yenu tena inasema mumepata habari kutoka kwa watu kwamba ni malalamiko, wale wanaongea hapa mimi ninaona kama wanaongea kwa njia mbaya tungesema kwa nini walituma hili jambo kutoka Nairobi.

**Interjections**: (inaudible)

**Kalasinga:** What? Democracy and I have also to talk, wacha na mimi niongee halafu msikie kwa nini walituma kutoka Nairobi.

**Nakholi**: Tafadhali ana haki ya kuzungumza mpatie nafasi tafadhali, wewe pia utapatiwa nafasi.

**Kalasinga:** Nasema hivyo kwa sababu wale walikaa chini walikuwa watu wa Trans Mara na sijui kama hapa kuna watu wa Trans Mara kuliko wengine, wale walikuja kukaa chini na kuchagua watu ni watu wa Trans Mara na walipewa haki kama ni constitution basi walikubaliwa; kama hawangeweza kukubaliwa hangechagua. Hiyo ndiyo mimi ninaongea kwa sababu mimi nimesikia wenzangu mkiongea ya kwamba hiyo kitu irudiwe, irudiwe kwa nini? Na walikubaliwa waongee. Kama kulikuwa na jamii moja ambao hawakuwa ndani ya hapo, how many people were there, tungeambiwa. So kama decision hiyo ilifanyika, hiyo decision ilifanyika siku hiyo wakachagua hao watu mimi ninasema ndio.

**Nakholi:** Hiyo tumesema tumeandika haya maoni na tunapeleka Nairobi wale Commissioners waone watafanya nyinyi, kwa sababu hii si ya kwanza, tulipata hii habari katika Narok South, tumeipata hapa na hatutawacha lazima tuandike maoni na tumeandika. Kwa hivyo tafadhali kama una hii tulia tuendelee na kazi, kama ni hii- sema tu hapo halafu tutafunga hii chapter.

**Speaker:** In other words we are asking which criteria the Commission from Nairobi ilisema kwamba the Council ndiyo inachagua watu?

**Nakholi:** Basi wacha nifafanue kidogo, hii hata si Commission ambayo ilifanya hiyo taratibu ya kuchaguwa watu, ilitoka Parliament. Parliament ndiyo ilipitisha ya kwamba, delegates kutoka ma-district ambao ni watatu, mmoja wao lazima awe ni mwanamke, ilitoka Parliament na ikatengenezwa huko ikaletewa Commission ili watu wachaguliwe kwa ile njia na watu watafanya Electoral College ni Councillors na sio wote bali County Councillors. Sasa haya mambo yote yalifanyiwa na watetezi wenu huko kwa Parliament ndiyo ikarudi. Kwa hivyo, tumesema tumeichukuwa hii ingawa sasa inasemekana au inakuwa kama tunafunga mlango wa nyumba kama ng’ombe imeshachukuliwa na wezi, kwa sababu sasa ninawasomea majina yako hapa na yamekuwa gazetted. Kwa hivyo tutachukua hili jambo liende liangaliwe tujue ya kwamba huko Narok South na hapa Trans Mara tumekuwa na shida. Tumesema ardhi imekuwa ardhi kati ya jamii za Maasai, jamii ya Kalenjin na ni jambo ambalo ni la muhimu sana na ni lazima tuwaonyeshe vile.

**Raria:** Asante sana Bwana Nakholi na ni matumaini yangu ya kwamba mumeshafungua sehemu ambayo inaguzia ardhi na mali na ningependa tu kudokeza ya kwamba ardhi katika nchi hii ya Kenya ni sehemu muhimu sana katika uchumi. Ni kwa sababu Wakenya wengi wamekuwa kwamba ukulima ndio umekuwa uti wa mgongo wa nchi hii na ukulima hasa inawezekana tu kufanyika kukiwa na ardhi. Kwa hivyo, katika nchi hii ni rasilmali muhimu sana na wananchi walionelea ni vizuri sana Katiba iguzie sera ya ardhi na ni kwa sababu kulikuwa na malalamiko nyingi sana ama shida ambazo zimetokana na ardhi ambayo

wananchi waliweka uzito, na bila shaka Katiba hii mpya iliweza kuguzia mambo hayo na kuweza kuibuka na sera kuhusu ardhi ambazo nitawaelezeeni hivi punde.

Lakini hasa shida ya ardhi ilianza kwa mbali sana, shida ya ardhi hata imeanzia hata tukiangalia historia tu, tukirejelea historia ndiyo tunaweza kujua hasa kiini cha shida ambazo zinatukumba hivi sasa kuhusu ardhi, kwa sababu, watu wa sehemu hii wanaelewa kwa undani mambo ya agreements zilizofanywa katika miaka za jadi. Miaka ya 1904 na 1911 kulikuwa na agreements, pre-independent land treaties, ambazo zilifanywa baina ya jamii za Kenya na wakoloni ama wazungu waliokuja kutumia ardhi yetu, na hizo agreements za umilikaji wa ardhi zimeendelea kudhuru wananchi hata kwa wakati huu. Na ndivyo basi wananchi wamesema jambo hilo la agreements ni sharti lirejelewe katika Katiba hii na wananchi wapewe suluhisho ili waweze kukaa katika ardhi yao, waweze kumiliki ardhi kwa sababu kila Mkenya anahitaji kuwa na ardhi iwapo anaweza kujimudu kiuchumi. Kwa sababu tulivyosema hapo awali, ardhi ni rasilmali na ardhi kwa kusema kweli ni mali, ina dhamani kuliko gari, ina dhamani kuliko nyumba, ina dhamani kuliko jambo lolote lile ambalo mtu angependa kujivunia. Kwa hivyo Wakenya wameonelea ya kwamba ardhi ingepaswa kuwa ni haki ya kimsingi kwamba kila Mkenya aweze kumiliki ardhi ili ajiendeleze kiuchumi.

Shida ambazo wananchi waliweza kueleza Tume ya Kurekebisha Katiba, wamesema hata miaka arobaini baada ya uhuru tungali tuna Wakenya ambao hawana ardhi kabisa na hawawezi kufanya kilimo kwa sababu ardhi imekuwa adimu. Ilhali Wakenya wanasema ya kwamba kuna Wakenya wachache sana ambao wanamiliki maelfu na maelfu ya mahekari ambazo hata ardhi zingine hawatumii na Wakenya wengine wengi sana hawana ardhi ya kuendelesha maisha yao. Basi Wakenya walisema hiyo ni shida kubwa sana ambayo ni lazima Katiba itoe mwongozo kuhusu hali ya kutatua shida hiyo na nitawaelezeni vile Katiba imeguzia swala hilo.

Pia Wakenya wamesema ya kwamba kupata stakabadhi za kumiliki ardhi ama title deed imekuwa ni ya gharama ya juu sana na pia process ya kupata stakabadhi ya kumiliki shamba inachukua muda mrefu sana. Kwa hivyo, imekuwa ni gharama kubwa kwa wakati na imekuwa ni gharama kubwa sana kwa hali ya fedha. Kwa hivyo, wananchi wamesema lazima kuwe na mpango kabambe ya kuhakikisha ya kwamba umilikaji wa ardhi na kupata stakabadhi ya kumiliki mashamba ni lazima iwe ni ya nafuu na ni lazima pia ikiwa umenunua shamba ama umepewa shamba lolote la kumiliki ni sharti stakabadhi ya kumiliki shamba hilo itoke mara moja.

Wananchi pia walionyesha kutoridhika kwao na sheria nyingi ambazo zinaguzia ardhi, kuna sheria nyingi sana, tuko na sheria sitini na saba ambazo zinaguzia juu ya ardhi na sheria hizo zote hakuna moja iko na uhusiano na ile nyingine. Kwa hivyo, sheria moja ikisema hii juu ya ardhi basi sehemu nyingine sheria iko na mapendekezo tofauti kuhusu ardhi, kwa hivyo kukiwa na sheria nyingi kama sitini na saba kuhusu ardhi basi yaonekana kwamba pengine shida ya ardhi inatokana na hizi sheria nyingi. Kwa hivyo, wananchi walieleza Tume ya Kurekebisha Katiba ya kwamba ni vizuri wakija na sera ama wakuje na sheria moja au chache zinazoguzia ardhi na ambazo zina uhusiano na zinaweza kufuatwa na kuelewa na kila mwananchi ili mwananchi akiweza

kumiliki sehemu yoyote ya ardhi basi ajue ako na haki na kumiliki na hakuna sheria yoyote nyingine ile ambayo mtu mwingine anaweza kutumia ili kumpokonya ardhi yake.

Pia wananchi walisema ya kwamba stakabadhi za kumiliki mashamba zinapatikana kwenye maofisi zilizo mbali sana. Aidha unapaswa kwenda katika jiji la Nairobi ili upate stakabadhi za kumiliki ardhi au uende katika headquarters ya Province ambayo pia inaweza kuwa mbali. Ningependa kuwapa mfano wa mtu anayetafuta stakabadhi ya kumiliki shamba, anayeishi Marsabit na wajuwa headquarter ya Province yake iko Embu, kwa hivyo, Mkenya huyo atalazimika kugharamika ili kuweza kuenda kadiri ya kilometer mia sita hamsini kusudi tu apate stakabadhi hiyo. Kwa hivyo, wananchi walisema ni sharti Katiba itoe muongozo wa kuhakikisha ya kwamba, stakabadhi ya kumiliki mashamba kwa sababu ni haki ya kila Mkenya, ni lazima iwe katika ofisi zilizo karibu sana, ofisi zilizo karibu nao na tutakuja kuzungumzia mambo ya usambazaji wa utawala ama devolution na mambo kama haya yataweza kushugulikiwa na maofisi ambazo Katiba hii imependekeza ya kwamba kutakuwa na serikali hata ya vijiji na mambo kama stakabadhi ya ardhi au shida zingine za kuhusu ardhi zitatoka katika sehemu za mbali na mtaweza kuhudumiwa katika maofisi ambazo ziko kati ya wananchi. Kwa hivyo, mtakuja kuona hiyo wakati tutakapoenda kuguzia mambo ya usambazaji wa utawala.

Shida ambayo imetokea pia kuhusu ardhi na ambayo wananchi walilalamikia sana, kulikuwa na kilio ya kwamba kumekuwa na mizozo mingi sana kuhusu ardhi, wananchi wamesema kwamba kumekuwa na vita kuhusu ardhi kwa sababu wananchi wengine wanasema wao ndio wamilikaji wa haki na wengine wanasema sisi ndio wamilikaji wa haki. Kwa hivyo juu ya huo utatanishi kumekuwa na mizozo kuhusu ardhi na kwamba wananchi wamesema kwamba maisha yamepotea, damu imemwagika na mali kuharibiwa na hata mazingira kuharibiwa kwa sababu kuna uchomaji wa misitu kutokana na mizozo hizi za ardhi na wananchi wamesema ni vyema kabisa tuwe na suluhisho la kudumu kuhusu shida hii ya mizozo ya mipaka na mizozo ya ardhi na mambo hayo ndiyo nitakayoenda kuzungumzia.

Pia shida kubwa sana ambayo imeweza kudhiri mipaka ni jambo la unyakuaji wa ardhi, land grabbing. Wananchi wamesema tabia hii ya unyakuaji wa mashamba imekuwa kama ni desturi ya Wakenya, wamesema ya kwamba mali nyingi sana ya serikali, rasilmali ya serikali imeweza kunyakuliwa. Wananchi wamesema kwamba sehemu kama vile vyoo vimenyakuliwa, pia wamesema sehemu za makaburi zimenyakuliwa, sehemu za kando kando ya barabara zimenyakuliwa, sehemu ambapo watu wanachezea ama playing grounds zimenyakuliwa na hata compounds za mashule pia zimeweza kunyakuliwa. Hivyo basi, kulikuwa na sera ya serikali kusema ya kwamba sehemu zozote za shule, shule zote zinapaswa kuyakagua compounds ili kuzuia wanyakuaji hawa ambao wanaonekana ya kwamba hivi karibuni kama hakuna mpangilio mzuri ambao utatolewa ama muongozo utakaotolewa katika Katiba hii wataweza kunyakuwa Kenya mzima na watu wengine watabidi kuishi kwa mwezi.

Basi wananchi wamesema ya kwamba hasa hawangependelea wanasheria waingilie mambo ya kusuluhisha mambo ya ardhi kwa sababu wamesema wanasheria wamekuwa wakiungana na kuweza kuungana na watu ambao wanafanya tabia hizo na kwa hivyo, wananchi hawapati haki wakati wanapolalamika ya kwamba sehemu zao za ardhi zimenyakuliwa. Basi wamesema ni

vizuri sana kwa surveyors wawe tu ndio wanahusika kwa mambo ya ugawaji wa ardhi ama kudhibitisha umiliki na wanahitaji pia kufanyiwa training ili waweze kuelewa shida za ardhi zinazowakumba wananchi.

Basi nilivyowaambia ya kwamba, hivi sasa shida hizi zote Tume ilionelea kwamba shida kuhusu ardhi inatokana na sababu ya kwamba serikali hivi sasa haina sera kuhusu ardhi. Kwamba government does not have a policy on land na kama serikali haina sera kuhusu ardhi, ndiyo sababu sheria nyingi zimeweza kubuniwa na mwananchi amekuwa akichanganyikiwa kwa sababu haelewi mapendekezo ya hizi sheria ambazo ni nyingi sana. Kwa hivyo, Tume iliweza kutoa sera kuhusu umilikaji wa ardhi na moja kati ya land policies ambayo commission imetoa ni kuwa Wakenya wote watahitajika kuwa na ardhi na kwamba kila mwananchi ataweza kupata sehemu kiasi fulani ya ardhi ili aweze kujiendelesha kiuchumi.

Kwa hivyo, Katiba hii imedhamiria kuhakikisha ya kwamba there is access to land to every Kenyan na hiyo ni sera moja katika mapendekezo ambayo Tume ya Kurekebisha Katiba imetoa Wakenya wote watahakikishwa ya kwamba wako na ardhi na sio ya kukodisha bali Katiba hii itahakikisha ya kwamba kila Mkenya ako na ardhi na atamiliki ardhi hiyo na atapata stakabadhi na hiyo stakabadhi italindwa na Katiba.

Kwa hivyo, sehemu nyingine ambayo sera hii imeguzia ni kuhusu kulindwa kwa haki ya kumiliki ardhi yako iwapo umenunua ardhi mahali fulani katika nchi, basi Katiba itamlinda mwananchi huyo ambaye ameweza kutumia mali yake kununua shamba au kununua mali nyingine. Kwa hivyo, iwapo umenunua ardhi mahali fulani katika nchi hii ama umenunua mali, lands and property hizo mali zote zitawezwa kulindwa na Katiba ili kila Mkenya mahali anapokaa asiwe na wasi wasi ya kwamba pengine kunaweza kutokea shida kwa sababu, Katiba hii itamlinda mwananchi huyo, mali yake na ardhi yake.

Pia katika sera ambayo Katiba imetoa kuhusu ardhi, wameweza kuhakikisha ya kwamba kutakuwa na matumizi bora ya ardhi hata ikiwa uko na stakabadhi ya kumiliki shamba fulani, Katiba hii inasema ya kwamba haupaswi kutumia ardhi hiyo vibaya unapaswa kulinda ardhi hiyo kwa sababu hata baada yako, ardhi hiyo itaweza kutumika katika vizazi na vizazi. Kwa hivyo, kuna sera mpya ya kwamba kila mwananchi na hayo ni mambo ambayo mtaona mkienda katika sehemu ya mazingira ya kwamba kila Mkenya atakuwa na jukumu ya kulinda mazingara.

Kwa hivyo, Katiba ilionelea ya kwamba ni vizuri hata ukiwa umemiliki shamba basi hupaswi kutumia shamba vibaya, hupaswi kukata miti ovyo ovyo ama kuchimba na kuwacha mashimo katika shamba lile. Ni lazima utumie kwa njia ya kwamba hata wewe kama huko pale, mtu mwingine ataweza kutumia.

Pia sera nyingine ambayo Katiba imeguzia kuhusu ardhi ni kwamba lazima kuwe na sheria kali ya kuhakikisha ya kwamba kama kuna ubadilishaji wa ardhi kupitia kununua na kuuza ardhi, jambo hilo litakuwa likifanyika katika njia wazi. Kwa sababu imeonekana ya kwamba wananchi wamekuwa wakifanya masikizano yao, mtu ukiwa na ardhi na unataka kuuza unaenda unaonana na mtu kwa siri halafu mnabadilishana pesa na kutoa agreements ambazo hakuna mtu mwingine anajua na hakuna ofisi

yoyote ya serikali inaelewa makubaliano yenu na baadaye kuna uwezekano wa kugeukwa. Halafu sasa hapo ndio unakumbuka ofisi ya serikali, sasa ndio nitaenda kwa ofisi ya Chief kwa sababu mtu amenigeuka nimenunua sehemu ya ardhi na sasa mwenyewe amenigeuka ameniambia ni lazima niongeze pesa, amenigeuka amesema hakuwa ameuzwa nilikuwa nimekomboa shamba hilo. Kwa hivyo, masikizano hayo ya siri hayatakubaliwa tena kwa hivyo, kutakuwa na muongozo wa kuhakikisha ya kwamba hata ubadilishanaji wa ardhi hata ikiwa ni yako ni lazima ihusishe ofisi ya serikali ambayo itahakikisha kuna ubadilishaji wa wazi kusudi shida isije ikatokea hapo baadaye.

Basi hizo ndizo sera muhimu sana ambazo Katiba ilitoa kuhusu ardhi. Na sasa jambo lingine ambalo nitaenda kulizungumzia ni juu ya umilikaji ama ownership of land, na hiyo inapatikana katika kipengele mia mbili ishirini na tatu katika nakala ambazo mko nazo. Land ownership imegawanywa mara tatu na jambo ningependa kuwakumbusha juu ya umilikaji wa ardhi, kuna tofauti kubwa sana kati ya Katiba tuliyo nayo hivi sana na Katiba ambayo wananchi wamependekeza sasa kuhusu umilikaji wa ardhi. Katiba tuliyo nayo hivi sasa inasema ya kwamba, umilikaji wa mwisho wa ardhi ni serikali. Hivyo basi hata wewe ukiwa na stakabadhi ya kumiliki shamba, uko na title deed, bado Katiba inasema ya kwamba wewe unaweza tu kumiliki hiyo ardhi hadi futi sita ambapo utaenda katika mapumziko. Na kutoka futi sita hadi vina vingine vya chini kule, ardhi hiyo ni ya serikali, kwa hivyo, hivi sasa hata mkiketi hapa kuna wale wako na stakabadhi za kumiliki shamba, shamba hiyo ama ardhi hiyo ambayo uko na stakabadhi ya kumiliki shamba bado ni ya serikali.

Na tofauti iliyoko na Katiba mpya ni kwamba inasema, 'ardhi yote si ya serikali tena bali ni ya watu wa Kenya ambao wanaishi kama jumuia, wanaishi kama communities ama watu ambao wako na title deeds ama kuishi kama binafsi basi ardhi yote ya Kenya itakuwa ya wananchi, aidha ukiwa uko pekee yako binafsi ambaye unamiliki stakabadhi ya kumiliki shamba ama kama jumuia unajua kuna sehemu zingine bado wanaishi kama schemes'. Kwa hivyo, bado hiyo ni sehemu ya kuonyesha pia umilikaji wa shamba. Kwa hivyo Wakenya wanamiliki mashamba either kama binafsi ama individuals ama katika majumuia ama communities. Kwa hivyo, hiyo ndiyo tofauti kubwa hasa baina ya Katiba mpya na Katiba tuliyo nayo hivi sasa.

Jambo lingine kuhusu umilikaji wa shamba, Katiba hii imebainisha wazi ya kwamba watu wasio wa Kenya hawawezi kamwe kumiliki mashamba. Katiba hii inasema ya kwamba ardhi yote ni ya Wakenya na watu wasio Wakenya hawana haki yoyote ya kumiliki ardhi katika taifa la Kenya ijapokuwa watu wanaoweka rasilmali wanaweza kushikilia ardhi ama wanaweza kukomboa ardhi kwamba 'non-citizens cannot own land but may hold or use lands on the basis of leasehold tenure for a period not exceeding 99 years'. Katiba hii inasema ya kwamba watu wasio Wakenya wanaweza ku-lease ardhi katika nchi hii na muda umepunguzwa hadi miaka tisaini na tisa pekee yake.

Wananchi mnajua ya kwamba kuna makampuni fulani katika nchi yetu ambayo yamepewa lease ya miaka mia tisa tisaini na tisa karibu karne moja na wananchi wamesema ya kwamba hiyo sio haki kabisa kumpatia mtu asiye Mkenya lease ya miaka mia tisa tisaini na tisa ni kama kumpatia huyo mtu ardhi hiyo milele. Kwa hivyo, Wakenya walisema ni lazima Katiba irejelee shida hii ya lease na kuweza kupunguza lease hiyo kwa sababu ilivyoko hivi sasa ni kwamba ni kama watu wamepewa lease ya miaka

mia tisa tisaini na tisa ni kama wamepewa ardhi hiyo kabisa. Kwa hivyo, Tume hii ilionelea ya kwamba muda huo upunguzwe hadi miaka tisaini na tisa. Na mgependelea kujua je makampuni hizo ama wawekaji rasilmali hao ambao wamepewa lease ya miaka tisaini na tisa iwapo Katiba hii itaenda kutimia basi, mambo yao yatakuwa namna gani?

Na ningependelea kuwaambia mfungue katika hizo nakala zenu nafikiri ni page 47 kwa hizo nakala mko nazo.

**Nakholi:** Arobaini na saba hapo chini kabisa mwisho.

**Raria**: Page 47.

**Nakholi:** Mwisho kabisa wa page 47, arobaini na saba chini kabisa ownership of lands.

**Raria**: Basi mgependa kujua hawa watu ambao wako na lease ya miaka tisaini na tisa baada ya kutekelezwa kwa hii Katiba, mambo yao yatakuwa namna gani? Na Katiba hii inasema ya kwamba, 'baada ya utekelezaji wa Katiba hii maslahi yoyote yanayohusu ardhi ambayo ni kubwa zaidi kipindi cha kukodisha cha miaka tisaini na tisa inayoshikiliwa na mtu asiyekuwa raia, itabadilishwa kwa kipindi cha kukodisha cha miaka tisaini na tisa isipokuwa ifutiliwe mbali". Katiba hii inasema ya kwamba, wawekaji rasilmali ambao wako na lease ya miaka mia tisa tisaini na tisa baada ya utekelezaji wa hii Katiba basi hizo miaka zitapunguzwa ziwe miaka tisaini na tisa na miaka za ziada ambazo watakuwa wamekatazwa hakutakuwa na fidia ama hakutakuwa na compensation. Kwa hivyo, baada ya utekelezaji wa hii Katiba basi miaka zitarudishwa kutoka mia tisa tisaini na tisa hadi tisaini na tisa na hakuna fidia kabisa.

Sasa kutakuwa na aina tatu, mnajuwa hata kwa Katiba hii kuna aina tatu za ardhi, umilikaji wa ardhi umegawanywa mara tatu. Katika Katiba tuliyo nayo hivi sasa na hata Katiba mpya imegawanya umilikaji wa ardhi mara tatu lakini kuna mabadiliko juu ya umilikaji. Ukiangalia kipengele cha mia mbili thelathini na nne kinaonyesha juu ya classification of land na kwa Katiba tuliyo nayo hivi sasa kuna government land ardhi ya serikali, trust land ambayo iko chini ya County Councils ama mabaraza ya miji, na private lands ama ardhi ya binafsi. Kwa hivyo, hata kwa Katiba ya sasa kuna classifications hizo kuhusu umilikaji wa ardhi. Lakini sasa kwa Katiba mpya kuna public land ardhi ya uma, kuna community land ardhi ya jamii, na private land ambayo itakuwa ni ya kibinafsi vile tu ilivyo katika Katiba tuliyo nayo hivi sasa.

Kwa hivyo, mtaona kwamba serikali haitakuwa ikimiliki shamba bali shamba hizo ama ardhi itakuwa ya uma na kwamba pia hakutakuwa na trust lands, itakuwa ni community land ama ardhi ya jamii na bado wale ambao hivi sasa wanamiliki mashamba wako na title deed, itabaki hivyo hivyo mtabaki na title deed zenu na zitatambuliwa katika Katiba mpya.

Basi ningependa kuwaambia juu ya description of public land ama public land ambayo tumesema ni ardhi ya uma itakuwa inahusu ardhi ama itakuwa inahusu sehemu zipi? Basi tumesema ardhi yoyote ambayo iko chini ya wizara yoyote, 'all land under any ministry ama under any department ama agency of government, yenye ardhi yote iko katika shirika lolote la serikali itakuwa ni ardhi ya uma.

Pia ardhi yoyote ambayo baada ya Katiba hii kutekelezwa hakutapatikana mwenyewe ama hakuna mtu anayemiliki shamba hizo, ardhi ambayo haina umiliki wowote basi ardhi hiyo itakuwa pia ni ya uma. Tumesema pia mabarabara na sehemu za kando kando za barabara zitakuwa pia chini ya ardhi ya uma. Na tumesema mito zote na sehemu za maziwa kuu zitakuwa pia ni ardhi ambayo itakuwa ni mali ya uma. Tumesema pia ma- bahari kama vile Bahari ya Hindi, tumesema ufuo wa bahari huo na hata chini ya bahari pia itakuwa ni mali ya uma.

Lakini mgependa kujua ardhi hii ya uma ni nani atakayekuwa ni mmiliki ni nani atakeye shikilia stakabadhi ya umiliki wa ardhi ya uma na pendekezo hilo liko katika kipengele ya mia mbili thelathini na tano 1 (a) na inasema ya kwamba, National Land Commission itaweza kuwa na stakabadhi ya kumiliki ardhi yote ambayo nimesema itakuwa ni ya uma. Basi kutabuniwa Tume ya National Land Commission, unajua sasa tuko na Land Commission lakini katika Katiba kutabuniwa Tume ya National Land Commission na hiyo ndiyo tunasema ya kwamba itakuwa ikimiliki ardhi yote ambayo inasemekana ni ardhi ya uma.

Community land ama ardhi ya jamii inapatikana katika kipengele cha mia mbili na thelathini na nne, na vile tulivyosema hapo awali ardhi yote ambayo hivi sasa iko chini ya County Council, ardhi ambazo zinaitwa trust land zitarudishwa katika jamii ambao wanaishi katika sehemu hiyo. Kwa hivyo, kama kuna ardhi yoyote ambayo inashikiliwa na County Council kama trust land katika sehemu za jamii fulani, basi mjue iwapo Katiba hii itaweza kutimia ardhi hizo za trust lands zitarudishiwa jamii ambazo zinaishi katika sehemu hiyo.

Pia group ranches zote ambazo ziko katika ndani ya jamii, hizo pia zitakuwa zikiitwa community land ama zitakuwa ni ardhi za jamii. Pia kuna ardhi zingine ambazo zinatumiwa na jamii ambazo mnaweza kukuta ya kwamba kuna sehemu fulani katika ardhi yenu ama katika jamii kuna sehemu fulani ambazo ziko gazetted lakini bado communities ama jamii zinatumia sehemu hizo kwa malisho ya mifugo wao ama kupata maji. Sehemu hizo ambazo ni gazetted lakini ziko katika area ya jamii basi ardhi hizo zitarudishiwa jamii.

Sina mfano mzuri sana katika sehemu hii lakini ninaweza kuwapatia mfano wa Namanga hills, sehemu ya Namanga hills ni gazetted lakini community ya hapo wanatumia kulisha mifugo wao wakati wa kiangazi na wananchi wa sehemu hiyo walisema ya kwamba, inapaswa sehemu hizo ambazo ni gazetted na zinaonekana ni ardhi za serikali, sirudishiwe jamii zinazoishi sehemu hizo kwa sababu wanatumia katika nyakati za shida.

Kwa hivyo, Katiba hii imeweza kutilia pendekezo hilo umuhimu na kusema ya kwamba ardhi hizo ambazo ni gazetted na kwamba majamii wanatumia katika shughuli zao, shughuli za malisho ya mifugo na kadhalika, hizo zitarudishwa kwenu, zitarudishwa katika jamii zinazoishi katika sehemu hiyo.

Pia jambo mgependa kujua ni kwamba ardhi hii ambayo tunaita ardhi ya jamii ama community land, mgependa kujua ni nani hasa atakuwa ana stakabadhi ya kumiliki ardhi hizo. Na katika kipengele mia mbili na thelathini na tano 2 (a) kuhusu tenure

ama hali ya umiliki inasema ya kwamba, baada ya hizo jamii kujulikana jamii hizo ambazo zimeishi hapo kutoka jadi, ikishajulikana baada ya utekelezaji wa hii Katiba na baada ya Bunge kupitisha sheria ya kuhakikisha ya kwamba ardhi zote ambazo ziko na mizozo zimeweza kugawanywa katika hali ya haki basi hizo jamii watapewa stakabadhi ya kumiliki ardhi hiyo ambayo inaitwa community land.

Pia kuhusu ardhi ya jamii, kutakuwa na sheria kali sana kusudi watu wachache wasiweze kukutana na waseme tutauza sehemu fulani ya ardhi ya jamii. Kwa hivyo, kutakuwa na sheria kali ili kulinda sehemu za jamii kwa sababu kuna watu ambao wamezoea mambo ya unyakuaji wa mashamba na kukiwa na ardhi ya jamii ambayo hakuna mmilikaji mmoja basi utakuta ya kwamba kutakuwa kati yenu na watu ambao wamejazwa na kasumba ya uporaji na wamejazwa na kasumba ya kunyakua mashamba, basi nyinyi mkiendelea na shughuli zenu watapitisha sheria fulani halafu wauze sehemu ya ardhi hiyo ya jamii. Kwa hivyo, Katiba hii inadhamiria kutoa sheria kali sana kuhakikisha ya kwamba ardhi ya community, ardhi ya jamii haitaweza kuuzwa ama kupeanwa kwa njia ambayo community hawajaweza kuketi na kukubaliana kwamba jambo hilo lifanywe.

Basi tumesema umilikaji wa tatu ni juu ya private land ama ardhi za binafsi na tumesema ya kwamba ardhi zote ambazo watu wanamiliki kwa ubinafsi na wako na title deed ama wako na stakabadhi ya kumiliki mashamba hayo, tunasema kwamba hizo ardhi ndizo zinaitwa private land na Katiba hii inatambuwa umilikaji huo. Kwa hivyo, watu ambao hata sasa wako na title deed Katiba hii inaapa kutambua watu hao ambao wako na stakabadhi za kumiliki mashamba na ni haki katika Katiba wewe ukiwa na stakabadhi hiyo na haki yako italindwa na Katiba pamoja na ardhi na mali ambazo umepata kwa haki, ni sharti ya Katiba kuweza kukulinda.

Pia kuna sheria kuhusu ardhi kwa sababu Tume ya Katiba ilionelea ya kwamba kuna shida fulani ambazo wananchi walizungumzia na kwamba kwa muda ambao Katiba ilipewa, shida zote kuhusu ardhi ambazo Wakenya walipendekeza hazingeweza kufanywa na Tume ya Katiba pekee yake. Kwa hivyo, Tume hii imepatia Bunge miaka miwili baada ya kutekelezwa kwa hii Katiba kuweza kupitisha sheria fulani kuguzia sheria zingine ambazo Tume ilionelea ni sensitive issues ambazo Katiba haingeweza kuja nazo na kutetanisha wananchi. Basi Bunge watapatiwa muda wa miaka miwili ili kushughulikia matatizo kama vile Wakenya walikuwa wanasema, je Mkenya yeyote anapaswa kuwa na kiasi gani cha ardhi? Basi Tume hii ilionelea ya kwamba kwa wakati huu hawangeweza kusema ya kwamba Mkenya anapaswa kumiliki kiasi fulani cha ardhi ama kuwa na limit ya lands, kwa hivyo, hiyo itapitishwa kwa sheria ya Bunge ambao watajadilia baada ya miaka miwili.

Pia mambo ambayo kuna mizozo ni kuhusu mipaka. Bunge pia watatoa sheria ya kuhakikisha ya kwamba mizozo kama hizo hazitakuwepo tena, na muhimu sana juu ya watu wa sehemu hii ni kwamba kuna hizi historical claims. Watu wa sehemu hii walilalamikia kwamba kuna sehemu za ardhi yao ambazo zilichukuliwa na watu ambao walinyakua ardhi yao hawakupata idhini kutoka kwa wananchi ama kutoka kwa jamii hizo. Kwa hivyo, ardhi hizo zinahitaji kushughulikiwa na kuhakikisha ya kwamba communities zimerudishiwa, kwa hivyo kuna hizo historical claims. Na pia kuna mambo ya ardhi ambazo zilitolewa kwa njia ambazo si za haki.

Kwa hivyo, wananchi walisema mambo za land treaties ambazo zilifanywa bila kupata idhini ya jamii basi hizo ardhi zilipatianwa kwa njia ambazo hazikufaa na wananchi walionelea ya kwamba Katiba hii ni lazima izingatie shida hizo. Na kwamba Katiba imesema ni lazima Bunge baada ya miaka miwili watoe mbinu ya kuweza kurejelea mambo hayo na Katiba imesema ni lazima Bunge wafikirie wanaweza kuenda miaka ngapi nyuma ili wajue hizo claims zilianza wakati gani. Ni kwa sababu kuna wananchi wengine wanasema ni vizuri Bunge waende hadi miaka za 1895. Wakenya wengine wamesema kutoka 1904 kwamba Bunge irudi nyuma tena ili iangalie historia ndiyo shida za ardhi ziweze kutambulikana kwa sababu niliwaambia, ili kuelewa shida hasa ambazo zinakumba wananchi hivi sasa juu ya ardhi, ni vizuri sana kurejelea historia ili kujua hasa ni kina nani waliokuwa wamilikaji wa haki.

Kwa hivyo Bunge katika miaka hiyo miwili itarudi nyuma na kuhakikisha ya kwamba baada ya kutambua shida mahali ilipotokea na kujua wamiliki wa haki wa ardhi hizo ambazo wananchi wanasema juu ya historical claims, Bunge likija na sheria na kutambua kwamba ardhi hizo zilipeanwa kwa njia ambazo hazifai, basi Katiba hii inasema ya kwamba kama ardhi hiyo ilipatianwa kwa njia ambayo si ya haki itaweza kurejeshewa wenyewe ama land kama hizo zitakuwa revoked.

Kwa hivyo, hizo ndizo sheria ambazo Bunge wataenda kutoa juu ya ardhi ili kuhakikisha ya kwamba, mbali na kuwa na usawa ama kuhakikisha ya kwamba Wakenya wote wako na sehemu ya ardhi pia kuna Wakenya wengine ambao wamelia ya kwamba, ardhi zao nyingi sana zimechukuliwa kwa njia isiyo ya halali na wanahitaji halali ifanywe na kwamba wanapenda kupata suluhisho ya kudumu kuhusu ardhi na kwa hivyo, Katiba hii

**George Nakholi:** Tukienda kwa mambo mengine tutaenda haraka haraka kidogo ili tumalize lakini tulitaka tuipe umuhimu ambao sasa imepewa. Sasa tutapata maoni au maswali kilingana na yale Bwana Raria amesema juu ya ardhi. Kama una swali lolote au jambo la kutupatia tuongeze kwa hii Katiba, sasa utakuja hapa mbele nikikuita utakuja hapa mbele useme jina, na utoe lile jambo.

**Speaker:** Nakushukuru kwa nafasi hii ili nami nitoe maoni. Tulikuwa tumesema ya kwamba zile titles ambazo zimepeanwa kwa sababu sheria ya sasa inasema ya kwamba title ikishapeanwa haiwezi kuwa challenged na tulisema ya kwamba ni heri sheria ibadilishwe ili titles nazo ziwe challenged kwa sababu ardhi ambayo imenyakuliwa ya watu wengine hawawezi kupeleka kesi kortini au kutoa uamuzi kwa sababu ile sheria inawazuia. Nafikiri nilisikia ikisemekana hapa ya kwamba ardhi mmilikaji amepewa mpaka futi sita chini na tunajua ya kwamba kwa Katiba ya sasa …

**Maurice ole Raria:** Kwa Katiba ya sasa mwananchi kutoweza kumiliki shamba mahali ambapo unaishi na vina vyote viko chini hata kukiwa na madini chini yake ardhi hiyo itakuwa ni ya mwanachi hadi kufika hekari elfu mbili chini, sehemu hiyo yote itakuwa yako mmiliki shamba na hata sehemu ya juu hadi kwa mwezi.

**Speaker:** Nafikiri hapo nimetosheka kwa kuwa hivyo ndivyo tulikuwa tunataka. Na hii mambo ya historical land ownership. Mimi nina tashwishi ya kwamba labda pengine bunge hata baada ya kupewa hizo miaka miwili labda hawatashughulika. Afadhali basi Katiba ieleze kinagaubaga ya kwamba kama bunge haitakuwa imetoa uamuzi kufikia hiyo miaka miwili then wananchi wenyewe wale ambao wanaclaim ardhi yao ambayo ilikuwa imenyakuliwa wapewe nafasi ya hata kupeleka mambo hayo kwa mahakama kuu ili yaamuliwe pale.

**Maurice ole Raria:** Na juu ya shida hiyo ambayo wananchi walisema ni vizuri kuwa jambo la title liweze kurudiwa ama liwe challengeable pengine katika Katiba hii, maneno hayo challengeable hayajawekwa katika Katiba lakini kuhusu jambo nilikuwa nazungumzia, juu ya sheria ambazo bunge itatoa na kuhakikisha ya kwamba iwapo kuna ardhi ambayo ilinyakuliwa kwa njia ambayo sio halali itakuwa revoked. Kwa hivyo pengine katiba haija tumia hasa yale maneno ambayo wewe umetumia lakini hiyo kipengele imepea kaitiba uwezekano Ya kuhakikisha ya kwamba hata kama uko na stakabadhi ya kumliki shamba, Katiba hii ukisoma kwa undani inasema ardhi, ama umlikaji wa shamba au wa mali ambao Katiba itaweza kukagua ni zmali ama ardhi ambao ulipata kwa njia ya halali kwa hivyo ardhi ambao umepata kwa njia ambayo sio halali hata ukiwa na stakabadhi ya kumliki shamba ni jukumu ya hii Katiba kuhakikisha ya kwamba title hiyo inaweza kuwa revoked.

**Stephen Ole Nguta**: Basi Bwana Commissioner na coordinator jina langu ni Stephen ole Nguta. Maoni yangu ni kwamba mambo yanoyohusu ardhi. Ulisema ya kwamba title deed lazima iwe na jina ya bwana na bibi sabavu watu wengi wamekosa mashamba sasa hivi kwa sababu shamba imechukuliwa na mtu mmoja.

Jambo langu La pili, kwa wale wasichana ambayo hawajaolewa, Katiba inaweza kuwapatia wao pia wapate shamba kutoka baba zao. Halafu jambo lingine Katiba inaweza kusaidia ni hiyo ranches. Katiba ya sasa pia iingie ndani kwa sababu tunaona tumefikisha miaka 39 ya uhuru wetu na mpaka saa hii kuna mashamba mengine ambayo hayajafanyiwa demarcation. Kwa hivyo katiba ichukue jukumu iharakishe kwamba hizo mashamba pia yaweze kufanyiwa mlikaji na wanaoishi pia wapate hiyo title deed. Hayo ni maoni yangu machache kuhusu mambo ya ardhi.

**Maurice ole Raria:** Hilo pendekezo la wananchi walisema ya kwamba ni vizuri kwa stakabadhi ya kumiliki shamba iwe na jina la mume na mke. Ni kwa sababu ikiwa hivyo wazee hawataweza kuwa na wakati rahisi wa kuweza kuuza ardhi hiyo kwa sababu itakuwa na wamilikaji wawili na itakuwa ni hali ya kulinda familia ama kulinda mali ya familia na jamii kwa jumla pamoja na watoto. Na ukiangalia katika haki za kimsingi ambazo hatuwezi kupitia sehemu hii yote ya Katiba lakini ningependa kuwaambia kwamba kwa mapendekezo ya Katiba hii kuhusu haki za kimsingi ukiangalia chini za haki ya kimsingi za kina mama ni kwamba watakuwa pia na haki ya kumliki mashamba, pamoja na watoto pia watakuwa na haki ya kumiliki ama kurithi shamba ya wazazi wao. Kwa hivyo wakati wako ukienda katika sehemu hiyo ya haki za kimsingi utakuta kwamba kina mama watakuwa na haki ya kumiliki mashamba ya familia.

**Paul ole Boini:** Wazee kwa jumla hamjambo. Naitwa Paul ole Boini na ningesema asante sana kwa hii commission kufika

hapa leo kutoa maoni hasa kutuelezea mambo ya ardhi. Kwa sababu hapa kwetu tumekuwa na shida kwa miaka 40. Kwanza mahali mimi naishi sasa hatujawahi kupata title deed, kwa hivyo sisi hatuwai kupata uhuru katika Kenya kwa maana ukiwa na title deed ya shamba, hiyo ni kumaanisha kwamba wewe uko na uhuru. Na kwa hivyo ukiguzia ile mlikuwa mnasema public ama shamba la community, kuna mashamba katika nchi za Maasai ambazo zilikuwa zimenyakuliwa na serikali kwa njia ambayo sisi hatujui na zilikuwa katika sehemu zetu, ilikuwa inaitwa ole miti na hayo mashamba yamechukuliwa yakapewa watu bila idhini ya wenyewe, hata sehemu za Narok hata sehemu za hapa, hata Kajiado. Hayo yalikuwa yanaitwa marketing board – livestock marketing trading grounds. Hizo sijasikia hiyo sheria ikiguzia hiyo na ni vitu ambavyo vilikuwa vya community na ni watu wengine wakakuja wakanyakua, kama hapa kwetu vice president alinyakua shamba letu na ni vizuri kama ingalikuwa sisi wenyeji tungerudishiwa hiyo shamba kwa sababu ilikuwa ni haki yetu. So zilikuwa sehemu zetu tukadanganywa na siasa hilo shamba likanyakuliwa.

Pia miaka arobaini iliyopita tumekuwa tukiteseka kwa ajili ya land control board pamoja na lands, yote, sheria za lands zote they are not even recorded hakuna records na ni mbaya kwa hivyo mimi ningalisema kwamba kwa shaeria ya hii Katiba ingetusaidia sana hasa waMaasai tupatwe hizo mashamba mara moja kwa sababu mimi nimeona hii sheria kama vile mumesema kwamba historical, ama baadaye tutakuja kuondolewa na mabunge sisi tutaangamia na ni mzuri kama mwakq ujua kitu ya kwanza sisi tunagawanyiwa shamba yetu kwa hivyo mimi sina lingine kwa sababu mimi sijapata title deed. Asante sana.

**Maurice ole Raria:** Mzee akilalamika ya kwamba bado yeye haja patata uhuru ni kweli kwa sababu ukiwa na title deed umepewa nguvu kwa sababu unaweza kutumia title deed hata kupata loan, kuwa security ya loan kwa hivyo inaawezekana ya kwamba kama mzee hana rasilimali ingine ama hana mali nyingine ya kuweza kuchukuwa hiyo loan basi bila hiyo tittle deed ni kama kwake haja pata uhuru ndio tunasema wakenya wanachukulia umulikaji wa ardhi kuwa ni jambo la muhimu na ningependa kuwahakikishia ya kwamba shida hii inaweza kuzungumuziwa sana katika Katiba kwa sababu imesema ya kwamba ni lazima ardhi zote ziweze kumilikiwa na wakenya na kwamba kutatolewa stakabadhi za kumliki mashamba. Kwa sababu hata kimesemekana ni sehemu ya jamii kama wananchi hawana stakabadhi za kumiliki mashamba basi hiyo shida haitakuwa imetatuliwa.

Na pia nilikuwa nimezungumzia mambo ya trust lands kama vile umesema LMD na ardhi zingine zilizokuwa zinashikiliwa na county council ama na department zozote ama agency ya serikali inasema kwamba ardhi hizo zinazopatikana katika sehemu ya communities ni lazima ziregeshewe communities. Na kwamba nilisema katiba hii italinda tu sehemu ardhi au mali ya watu ambayo ilipatikana kwa njia ya halali. Kwa hivyo kama kuna mtu anamliki ardhi fulani katika sehemu ambayo jamii inaishi na wananchi ama jamii inayoishi hapo wanaonelea ya kwamba hawakuhusishwa katika kuuza ama kupeana kwa hiyo ardhi, basi hiyo nilisema ya kwamba Katiba hii inasema ardhi hii ambayo haijapatikana kwa njia ya halali na haijapeanwa na jamii kwa njia ya halali basi ardhi hiyo au title hiyo itakuwa revoked na kurudishwa katika community.

Jambo ambalo ninaweza kunakili na kupeleka kwenye commission ni hiyo shida ambayo inasema bunge ikipatiwa muda

wanaweza kuenda pale na hawaoni kama hiyo ni shida muhimu inayowakumba wananchi na wanaweza kuchukua muda mrefu wakishughulikia mambo ya ardhi na kwamba munataka kukatwa kwa mashamba ya haraka. Hilo ni jambo ambalo nimenakili na tutahakikisha ya kwamba tukifika katika commission tutawapelekea commissioners ili waweze kujadiliana juu ya hilo jambo kwa sababu wanakutana tarehe 28 ili waweze kujadilia hizi habari ambazo zinatoka kwa wananchi kuhusu Katiba ambayo wameshasoma na mapendekezo ambayo wameona ni lazima kuwe na vipengele ili Katiba hii isikae bila kulinda maslahi ya wananchi wote. Kwa hivyo hizo shida za mashamba tutahakikisha kwamba zitafika kwa macommissioners.

**Jonathan ole Sialo:** Kwa majina ninaitwa Jonathan ole Sialo. Mimi ni chief. Mambo yangu ni matatu. La kwanza ni jambo la land ownership. Zaidi ni hili jambo linasema kila Mkenya lazima awe na ardhi. Hiyo itategemea mtu kutoka area gani kwa sababu ninapozungumza ama ninapowaza sehemu zingine za Kenya, ninajua pengine kesemekana mtu apate ardhi, wengine hakuna pahali watapata maana tayari imejaa hata hakuna nafasi. Na nikiona naona kama ile area ambayo itakuwa na nafasi ni area mimi natoka ambayo mimi nasema itategemea sisi Wamaasai kwa mfano tubebe mzigo wa Wamaasai ambao hawana ardhi tujue watapata kivipi ama wawe na haki ya kupata ardhi kwa upande wa Maasai. Na pia kila kabila ingine katika Kenya maana tuko na tutatumia hiyo, pia wajitafutie kule kwao mpaka haki yao ipatikane kule.

La pili ni hii mambo ambayo imesemekana tuwe na usawa kwa kumiliki shamba ama kiasi cha shamba. Mimi napinga hiyo kwa sababu mimi najua ya kwamba in other communities in Kenya watu wanaown half an acre and ni kitu ambacho sio cha maana kusema hata mimi pia Maasai nipimiwe nusu hectare tuwe na usawa. Hiyo mimi nasema hiyo itegemee pia katika jamii za kenya mzima. Kama sisi Wamaasai tuwe na haki ya kuown 3000 acres and above kwa sababu tuko nayo.

Halafu hii mambo ya owning of land. Kwamba sasa kutoka chini mpaka mbinguni ni how many kilometers chini mimi napinga hiyo. Mimi nasema hiyo sheria ambayo inachunga hiyo ibaki vile ilivyo kwa sababu ya kitu kimoja. Tukisema namna hiyo basi nchi yetu haita kuwa na faida yoyote kwa sababu kama shamba langu lina gold ndani na mimi ndio ninatawala hiyo gold mpaka sasa inabakia mimi ama community, then serikali haitakuwa na utajiri. Tutakuwa tumenyima nchi yetu utajiri na pia hii mambo ya kusema group ranches mimi naonelea ibaki vile iko kila siku kwa sababu inakuwa kwa manufaa ya jamii. Na kama haikuwekwa namna hiyo vile ilivyo hiyo sehemu ingekuwa grabbed na watu werevu kama haingekuwa sio hiyo trusts lands hiyo ilikuwa imewekwa.

Kwa hivyo mimi nasema hiyo ingebaki namna hiyo na iangaliwe sana kwa sababu italete shida tukisema kwamba iwe owned na watu ama some individuals ama community fulani, hiyo itakataza ***inaudible*** pengine kwa councils ama kwa nchi. Hii mambo ya utalii ambayo watalii wanakuja kutoka nchi zingine wanakuja for example hii Mara, itakuwa hiyo pesa haitakuwa ya serikali, itakuwa ya group ranches na naona kama italeta matatizo kwa nchi. Na msisahau ya kwamba the same government is paying us salaries, the same government inatupatia kazi nyingi kwa hivyo hiyo napinga nasema ibaki vile ilivyo.

**Maurice ole Raria:** Asante sana Bwana Jonathan Sialo kwa mapendekezo yako. Jambo nimeona ni kwamba wewe ni

mazalendo kabisa kwa sababu unasema ya kwamba ukiwa unamliki ardhi hadi vina vya chini na pengine kuna madini kwamba tunaweza kataza serikali mali na ilhali serikali inatekeleza jukumu fulani basi hiyo ni maoni yako na bila shaka tumenakili. Na kuhusu jambo hili la kusema kuwe na usawa wa ardhi ukiangalia ama kulingana na mjadala ambao macommisioner walikuwa nao kuhusu kipengele hicho cha kusema lazima Wakenya wote wawe na sehemu sawa za ardhi, kuna mapendekezo mengine ambayo ni lazima yazingatiwe kwa sababu haisemi tu usawa wa ardhi ni vile hali ya hekari vile iko tuseme lazima kila Mkenya awe na hekari 1000 kwa sababu kuna pia issue ya land carrying capacity kwa sababu saa hii tukiangalia katika sehemu ya Maasai area ambayo ni ya hekari 100 na ukiangalia sehemu katika Kiambu district ambayo ni quarter ya hekari utakuta hekari quarter kwa Kiambu iko na dhamana sana kuliko hekari 100 katika Maasaini ama nchi hizi kame. Kwa hivyo wakisema kwamba kuna equal access to lands, mambo kama hayo pia yanazingatiwa. Kwa hivyo haimanishi tu ni vile mchoro katika ardhi. Kuna pia mambo ya land carrying capacity ambayo Katiba hii imezingatia. Kwa hivyo msifikiri ya kwamba Katiba hii itasema ya kwamba ni lazima kila Mkenya awe na sehemu kama hekari kumi, sio hivyo inamaanisha katika Katiba hii.

Kwamba, tena Katiba hii, inatambua ya kwamba kuna wakulima wengine ambao ni wafugaji. Kuna wakulima wa Kenya ambao wanalima na kuna wafugaji. Na kwamba, hauwezi ukasema ng'ombe anaweza kujitosheleza katika hekari fulani, kwa sababu hata kuna sehemu zingine ambazo wafugaji huwa wanatenga kwa sababu ya wakati wa kiangazi, wanatenga sehemu hizo kwa sababu ya mifugo wengine wadogo kama vile ndama ama mbuzi. Kwa hivyo msione ya kwamba kipengele hicho kama vile kinasema kuna usawa kwa kumiliki ardhi msichukulie hilo jambo juu juu, kwa sababu kuna hilo jambo la land carrying capacity kwa hivyo hiyo ndio sababu tunasema bunge litapitisha sheria fulani ili kuhakikisha mambo haya yatabainishwa kwa wananchi na yataonyeshwa wazi wazi.

**George Nakholi:** Ukiangalia kipengele hapa cha hamsini kwa u kurasa wa nane kwa hiyo pull- out ulikuwa unasema upande wa kila mtu watu wengine wasije wakaingiliwa, hiyo ni sawa imeangaliwa kwa Constitution lakini ukiangalia kwa hiyo inasemekana hapo 51 ukurasa wa nane, kila mtu ana haki ya kuenda mahali popote, ya kuwacha Kenya na kuenda nchi vile anataka na kila mtu ana haki ya kukaa mahali popote Kenya. Number tatu. Kwa hivyo imeangalia kama wewe ni Mkenya, ni Mkenya kama vile utangulizi unasema, preamble. Sasa wewe una haki chief Jonathan kutoka hapa na uishi Kakamega. Na mtu anna haki kutoka Busia pia akuje aishi hapa Transmara akinunua shamba. Lazima anunue au apate kwa haki.

**Paul Koi:** Wananchi hamjambo, langu ni fupi sana. Ninarudia maneno ambayo chief amesema kwamba, group ranches should remain the same. Mimi nimesema hapo mbeleni ya kwamba mimi sijakatwa mguu. Usifananishe mimi ambaye niko na taabu na wewe uko na title deed. Hata ingawa tuko na group ranches ama tuko na mahali ambapo wanyama wanakaa tuseme parks, hizo parks lazima hata hiyo inaguzia kwa hii katiba. mlisikia kwamba hizo zinakuwa katika, community. Community ndio inaown hizo parks na kwa hivyo ile kitu ninasema hata wakati Commission of Lands ya Njonjo ilikuja tulizungumzia zaidi mambo ya lands. Hata bwana DC anajua mambo ya lands hapa ni shida na hata tukisema kwamba bila kukatwa ikae vile ilikuwako basi hata macommissioner hakuna kitu wamekuja kufanya hapa. Kwa hivyo mimi nafikishia hapo mukijua macomissioners mukirudi kwamba issue ya Transmara niland ikatwe. Asante sana.

**George Nakholi:** katika huo mkutano wa 24 ichunguzwe, iende kwa National Constitutional Conference kutokana na yale mambo, na wale watatu ingekuwa vizuri kama wangekuwa hapa pia wasikie kabisa. Mmoja amekuja? You are a delegate? If you are hearing the views of the community about the group ranches, so you are hearing and this must be put into focus at the conference.

**Johanah K. Chirchir:** Asante sana Bwana Commissioners ambao wametembelea sisi hapa na wananchi wote kwa jumla. Kwa majina mimi naitwa Johanah Kiprotich Chirchir. Kitu mimi nataka kuguzia ni mambo ya unyakuzi wa ardhi. Sijasikia katika kwa maoni yenu ya kwamba a land grabber anatakiwa afungwe zaidi ya miaka kumi ili kila mwananchi apate nafasi ya kuishi. Katika Transmara land, grabbing is very high. Unakuta mtu, high court judge, anakuja kunyakua ardhi ya wananchi, DC anakuja kunyakua ardhi ya wananchi. Na ukienda kortini utafaulu kweli? Na kwa hivyo tunaomba commission ipitishe sheria ya kwamba yule mwenye kunyakua afungwe. Tumepata taabu sana katika Transmara.

Kwa mambo ya group ranches, wanakamati wametumia sheria ya group representatives act kuuza ardhi. Unakuta committee ako na mamlaka ya kupea kila mtu shamba vile anapenda tu. Hata kama members wamepitisha sheria ya kwamba tutakata hii shamba namna hii, namna hii anawacha hiyo na ana tumia hayo mamlaka kuuza haki na ndiyo taabu sana katika Transmara. Na kitu ambacho tunaomba mambo ya evictions baada ya kukata shamba, mtu amekuja kunyakuwa shamba kama ni high court judge anaenda kwa DC anaeleza DC toa kuna watu ambao wanaishi shamba langu na DC anakuja na kutoa wale watu hawana chochote halafu yule mtajri anakuja kuishi hiyo shamba. Hayo mambo ya evictions yaangaliwe. Asante sana.

**Joseph Koech:** Kwa majina ni Joseph Koech. Kitu ninaguzia ni the limit of acreage mtu anafaa ashikilie katika Kenya. Hiyo ni maoni yangu. Vile vile sijasikia watu wakiguzia miaka ngapi ambayo mtu atachukua ili amiliki hiyo shamba because katika Transmara sisi Wakalenjin tunaitwa we are land grabbers na sisi tumekaa hapa since 1954 mpaka saa hii. Sasa hiyo kitu tunaona it is good to state the years zile mtu anafaa akae kwa a certain place halafu apewe shamba. Thankyou.

**Maurice ole Raria:** Thankyou, kwanza ningependa kusema ya kwamba ni vizuri sana kama kuna mtu atakuja kutoa maoni yake kwa sababu hii Katiba imeandikwa na mamilioni ya wananchi na kila mtu alikuwa na nafasi yake ya kuzungumza kwa hivyo tafadhali vile wewe ulipatiwa muda wako wa kutoa maoni pia mpatie mwenzako kwa sababu tuko katika mjadala na tutaandika hii Katiba kwa mazungumzo na kwa kuelewana. Kwa hivyo jambo ningependa kusema juu ya Koech ni kusema ya kwamba ijulikane ni muda gani mtu anapaswa kuishi katika sehemu ili aweze kuwa mmilikaji wa ardhi, hilo ni ono ambalo ni jipya sana na ni jambo muhimu sana ambalo umeguzia na bila shaka hii itapewa upeo wa mbele wakati macommissioners wataenda kuzungumza tarehe 28. Ni jambo geni sana hatujasikia kwa sehemu ambazo tumeshaenda, hatujasikia pendekezo kama hili na kwa hivyo tunakushukuru sana kwa kutoa oni ambalo ni la muhimu sana.

**Nicholas:** Kwa majina ninaitwa Nicholas. Mimi maoni yangu, kwanza kabisa ni kusema ninahofia sana vile hii Katiba

inaendelea. Kwa sababu jambo la kwanza ukiangalia kipengele cha 232 sehemu ya pili (a) utapata hapa katika yale mapendekezo yetu ya watu wa Transmara, kuna jambo ambalo limeandikwa hapa kuwa ati tulisema kila Mkenya apate ardhi mahali popote ama wapate ardhi sawa na wengine na hiyo mimi ningependa kukanusha hiyo kuwa hatukusema jambo kama hilo.

Jambo la pili ni kuhusu ile Chief Ole Sialo alisema ardhi kama ile Maasai Mara ibaki chini ya wenyewe watu wa Transmara lakini isisimamiwe na serikali. Rasili mali yote iwe chini ya watu wa Transmara.

Jambo la tatu ni kuhusu umilikaji wa ardhi kwa sababu hatujaona katika hayo mapendekezo kuwa mtu wa Kiambu akisema wapate ardhi sawa wang'oe majani chai ama kahawa wapate ardhi huko ni kama hii Katiba inaelekeza macho katika ardhi ya zile communities ambazo watu ni wachache.

Ukiangalia pia hii Katiba ni kama watu wa Narok, Kajiado na Transmara hatujapewa nguvu na hii Katiba kuhusu mambo ya ardhi kwa sababu haijatetea sisi. Kwa mambo ya umilikaji wa ardhi. Ni kama inalenga watu wakubwa wakubwa kukuja kugrab ardhi upande huu, wakikaa kwa muda kidogo wanasema tupewe ardhi kwa sababu sisi ni Wanakenya na tumeenda kuishi mahali hapo kwa huo muda. Asante sana.

**Maurice ole Raria:** Kwa sababu mimi ni mmoja wenu na ninajua kwa kusema ukweli kwa Wamaasai Katiba kwao ni kama ni ardhi, kwa hivyo kama mambo ya ardhi hayajaguziwa basi Wamaasai wanaona kwamba wametengwa, hakuna Katiba. Lakini ningependa kuwahakikishia ya kwamba Katiba hii haisemi ya kwamba, pendekezo ama kipengele kinachosema ya kwamba Wanakenya wanaweza kumilika ardhi mahali popote. Katiba hii haijasema ya kwamba kutakuwa na uvamizi wa mashamba kama munavyo ona katika nchi ya Zimbabwe. Haijasema ya kwamba watu wenye ardhi lazima wavamiwe na wale ambao hawana ardhi waweze kunyakua.

Jambo hili lilikuwa limezungumuziwa hapo awali na tulisema ya kwamba wale watu ambao wanaweza kuishi katika sehemu nyingine ni watu ambao wanakuja kunua ardhi ile kwa njia ya halali na haijasema ya kwamba kutakuwa na uvamizi wa mashamba ya watu wanaoishi katika sehemu kame. Nimesema ya kwamba ni jukumu la serikali kuhakikisha ya kwamba hata wale watu ambao hawana ardhi ama squatters ni jukumu la serikali kupitia tume ambayo itaundwa ya National Land Commission kujua hawa masquatters au watu ambao hawana ardhi ni juu ya serikali kujua ni vipi hawa watu either watapatiwa ardhi ama wapatiwe fedha ili waweze kununua mashamba. Kwa hivyo haijasema ya kwamba ardhi ya Maasai ama sehemu hizi za Kajiado, Narok na Transmara ambapo bado inadhaniwa kwamba ina ardhi kubwa, hakuna kipengele katika Katiba hii inayopea jamii ambazo ziko na nguvu kuweza kuvamia ardhi ni ya Wamaasai.

Kwa hivyo ningependa sana musome hii Katiba kwa umakini sana kwa sababu sikubaliani na wewe ya kwamba haijasema kabisa mambo ya ardhi vile mapendekezo ya Wamaasai yalikuwa. Kwa sababu vile tuliongea hapo awali ni ya kwamba jamii

zote ama watu wote wanaomiliki mashamba ama wanaomiliki mali ni sharti kwa Katiba hii kuhakikisha itatoa ulinzi katika jamii hizo kuhakikisha ya kwamba ardhi yao italindwa na hii Katiba. Kwa hivyo hakuna mtu yeyote yule ambaye atatoka sehemu yeyote na kuweza kufanya jambo kama hilo la kuweza kuvamia mashamba ya jamii hii na kuwapokonya. Lakini iwapo wewe utapendelea kuuza shamba lako na mmefanya hivyo. Mmewahi kukubali jamii hizi kuweza kuja kununua mashamba katika sehemu zenu mtu basi atakuwa na haki ya kuuzia shamba lako mtu ambaye unamtaka. Kwa hivyo ile nguvu ambayo Katiba hii imezingatia ni kwamba mtu anaweza kuishi sehemu fulani lakini si kuenda halafu kusema mimi nitajikuta hapa lakini atazungumza na wenyewe aulize kama ni vyema akinunua shamba hilo na akinunua kupitia makubaliano basi itakuwa ni haki.

Pia umesema kwamba watu wa Transmara hawakusema ya kwamba Wakenya wanaweza kuishi sehemu yoyote ya nchi. Na ningependelea kuwaambia kwamba wakati wa kutoa maoni kulikuwa na yale maoni ambayo yalikuwa yanatolewa katika kikao kile ambacho Macommissioner walikuwa wanaketi na kuna maoni mengine ambayo yalitumwa kwa njia ya barua pepe ama kupitia internet, e-mails, zilitumwa kwa commission na kuna watu wengine pia walileta moja kwa moja kuja kutoa mapendekezo yao. Kwa hivyo mkiona maoni kama hayo yako katika hiyo report ya Transmara msiseme hatukusikia ama hatukutoa hayo maoni kwa sababu kuna watu wameandika barua zao kwa siri, pengine walikuwa wanahofia ama walikuwa hawana ujasiri wa kutoa maoni hayo katika kile kikao na wakahakikisha wameandika mabarua na kutuma katika commission. Kwa hivyo haikuwa pendekezo la commission kuweza kubagua maoni yoyote ambayo yanatolewa na mwananchi anayeishi hapo. Na nina hakika katika Transmara ijapokuwa wale wamezungumza hawapendelei pendekezo hilo kuna watu wengine wanapendelea lakini pengine hawawezi kusimama katika jukwaa hili na kusema kwa sababu wanahofia wingi wa watu ambao wanapinga pendekezo hilo.

Kwa hivyo mkiona maoni yoyote ambayo hamkusikia wakati ule usikuje kupinga kusema hatukusikia wakati ule kwa sababu kulikuwa na mbinu nyingi sana ya kutoa maoni. Haijakuwa report kamili mpaka uzungumze na ile committee ambayo itakuwa tarehe 28. Utapata ya kwamba commission iliangalia sana masilahi ya marginalised communities kama Wamaasai kwa sababu walijua tuko na loopholes kwa watu wenye kuingilia. Wanaona hii land ni kubwa, tunaweza kufanya kitu gani tuiingie. Waliona kabisa ndio wakatoa. Ukiangalia sana uende chini uangalie utapata kuna hayo mawaidha walitoa kuziba zile mbinu za watu wengine kuingilia ikianza kufanya kazi. Nenda usome na utapata hiyo ndani.

Kusema kweli kulikuwa na pendekezo katika mjadala wa macommissioner. Walisema kwamba kuna watu wakitembea au wakipitia mabarabara kupitia sehemu hizi za Transmara na Narok na Kajiado watu walikuwa wanafikiri kuna idle land. Na katika mjadala huo macommisioner kwa kauli moja waliamua ya kwamba hakuna idle land kwa sababu watu wanaishi sehemu hizo ama wafugaji hata sehemu zingine za North Eastern ambapo kunaonekana unaweza enda mahekari nyingi bila kuona mtu anaishi pale. Basi commission walionelea kwamba watu wasiwe na hiyo hisia ama wasiwe na hiyo mentality ya idle land. Wamesema ya kwamba katika sehemu hizi ambazo wafugaji wanaishi, wao huwa na sehemu kubwa ya ardhi kulingana na hali ya maisha yao. Wao ni wafugaji na wanahitaji sehemu kubwa ya ardhi. Kwa hivyo hiyo land sio idle kwa sababu iko na matumizi ya malisho kwa hivyo usifikirie jambo kama hilo la idle land lilifutiliwa mbali na commission. Asante.

**David Kaikai:** Kwa majina ninaitwa David Kaikai. I have a problem with……………….
Tuende katika kipengele 237, establishment of National land Commission. Pendekezo langu hapo ni kwamba wakati ambapo commission hii itaundwa, lazima kila kabila iwe imewakilishwa kwa sababu tumeona ya kwamba watu wengine wananyanyaswa kwa ajili watu wao hawako hapo. Kwa mfano wakati tuko na mambo ya Land Control Boards wale watu ambao ni members unaweza kukuta wengine hawajui ni nini hiyo Land Control Board inafanya. Na wengine hawajui kusoma, wanaenda tu kiuona mambo yamepitishwa hapo na yale mambo ambayo yamepitishwa hapo ni ya kumaliza wale ambao walikuwa wanahusika. Kwa hivyo wakati National Land Commission inaundwa tafadhali kila kabila ihusiswe. Kama ni Maasai, lazima Maasai awe hapo alinde masilahi ya Wamaasai kuhusu mambo ya ardhi.

Jambo la pili ni mambo ya urithi. Ilikuwa imesemekana utamaduni wa kila kabila lazima uheshimiwe. Wakati tunapoenda urithi wa shamba lazima utamaduni wetu wa Kimaasai uheshimiwe pia. Kulingana na sisi, msichana hana haki ya kurithi shamba kwa sababu fulani. Na tukisema hivyo tukipea wasichana warithi mashamba wengine wanaweza kuolewa huko na bwana wake halafu anarudi kuclaim hii shamba, na hiyo itaweza kuincrease prostitution ambapo mtu ataweza kuzaa akijua kwamba atapata shamba la baba yake. Kwa hivyo utamaduni wetu wa Kimaasai wakati unapochunga masilahi ya wasichana tafadhali lazima pia sisi tupewe kama jamii tujue namna tunaweza kuchunga hawa wasichana.

Kwa mambo mengine kuhusu mashamba ambayo tuliwacha, sisi tumetoka Uasin Gishu huko juu, kuna ADC farms lakini kitu cha maajabu hizo ADC farms zimechukuliwa na watu wakubwa wa serikali. Hakuna siku moja tumesikia watu kutoka Transmara wameitiwa shamba waende wagawe ADC farms. Kuna Enturai farm hapo Naivasha, ilikuwa yetu lakini watu wamevamia. Hata ninakumbuka minister mwingine wa zamani alibeba watu wake kutoka hapa hadi huko, akajaza huko. Wamaasai kufika huko wanashambuliwa kupigwa na hilo shamba lilikuwa letu. Kama ADC farms ziko na ile tulikuwa tunasema claims. Wakati hizo claims zinakuja, tafadhali kama bado kuna ADC farms ziko Kitale, Eldoret na pahali pengine Wamaasai wakumbukwe kwa sababu hizo shamba zilikuwa zao.

Halafu mambo ya sheria sasa ya shamba. Lazima sisi tupewe nafasi wakati ya kumiliki hiyo sheria na kutunga hiyo sheria kwa sababu tukitungiwa sheria hiyo na hatukuhusishwa na every step inachukuliwa kutunga hiyo sheria itakuja kutuaffect sana. Basi kwa hayo machache nasema asante sana.

**Maurice ole Raria:** Bwana David Kaikai, kusema ukweli mapendekezo yako ambayo umetoa. Mapendekezo yako ni muhimu sana na ingekuwa ni pendekezo langu pia kwamba hayo maneno vile umeyaweka namna hiyo ningependa pia uandike chini na upitishe through district coordinator halafu haya maoni yafike katika commission kabla ya tarehe 22, kwa sababu maneno haya ndio tulikuwa tunataka kuja kusikia kutoka kwa wananchi na mimi naona haya maneno manne ambayo umeyazungumzia ni ya maana sana.

Na kusema ukweli, jambo la kwanza ambalo ulizungumzia juu ya kwamba wakati wa kubuniwa kwa Land Commission ni vizuri kuwe na representatives wa communities ambazo wako na ardhi, ni ya haki kwa sababu kuna wananchi wengine walikuwa wanasema katika sehemu zingine ambazo pastoralists ama watu ambao wanamiliki mashamba wako walikuwa wanasema, ni lazima kwa sababu Wamaasai ni stakeholders katika land basi ni lazima wawe katika hiyo commission. Na wanasema ya kwamba katika coffee board basi ni vizuri pia kuwe na watu wa Kiambu kwa sababu ni stake holders in that field. Tea board ni lazima kuwe na watu kutoka sehemu ile kwa sababu walikuwa wanasema kwamba Maasai akiwa katika coffee board ama akiwa katika tea board na hajui mambo ya kahawa basi itakuwa ni a job for the boys. Na hilo jambo hata lilizungumziwa sana kwa upande wa Kajiado. Kwa kusema ukweli walikuwa wanasema hatutaki national land commission, tunataka land commission katika districts. Walisema ni lazima kwa sababu katika spirit ya devolution ambayo tutazungumzia hivi sasa, kwa devolution wananchi wa Kajiado walisema ya kwamba hatutaki hiyo national kwa sababu haituhusishi na kwa sababu national land commission ni kama tu kubatiza land commission kwa sababu bado tuko pale na wananchi walisema kwamba hatutaki national land commission, tunataka hiyo land commission katika sehemu za districts kwa sababu ndio inajua shida za wananchi. Kwa hivyo nikijaribu pia kuona mapendekezo yako yanahusiana na hiyo, bila shaka tumenakili ni muhimu sana.

Pia mambo umesema juu ya ADC lands ambazo zimenyakuliwa. Nilikuwa nimeongea hapo awali pia kuhusu mambo ya hizo lands ambazo zilikuwa chini ya county councils na mambo ya trustlands, mambo ya hizi ADC na LLD ambayo imezungumziwa pia. Tulisema ardhi hizo zote ambazo zilinyakuliwa ama zilipeanwa bila idhini ya wananchi nataka kurudia hii tena kusema ya kwamba it's challengeable katika Katiba hii inasema ya kwamba hizo ardhi zote ambazo zilitolewa kwa njia ambazo hazifai ama njia isiyo halali, Katiba hii haitalinda ardhi au mali yoyote ambayo imetolewa kwa njia isiyo ya halali. Kwa hivyo pamoja na Enturai farm na zingine ambazo ninajua ni vizuri sana muweke orodha zote na mtoe historia kuhusu sehemu hizo ambazo muko na shida nazo na mpeane katika commission kwa sababu pendekezo la Katiba hii ni kuhakikisha ya kwamba hiyo ardhi ni lazima wenyeji wa halali watambulikane na warudishiwe ardhi yao.

Jambo ambalo linatatanisha sana ni kuhusu urithi kwa sababu umesema ya kwamba utamaduni wa jamii ya Wamaasai inakataza urithi wa wasichana ama watoto wa kike kurithi ardhi, na kwa kusema ukweli nilikuwa nimesema awali kwamba Katiba hii pia inatambua utamaduni wa wananchi. Lakini inatatanisha ni kwa sababu Katiba hii imesema ya kwamba haki ya kila mwananchi akiwa ni mtoto wa kike, akiwa ni mama kuna usawa wa hisia katika katiba hii. Na Katiba hii inasema ya kwamba tamaduni ambazo zilikuwa zinadunisha kina mama, watoto wa kike, tamaduni ambazo kwa maisha ya sasa hayana maana tena ama discriminatory aspects of culture, tamaduni ambazo hazituletei maendeleo, ni vizuri sana jamii ya Wamaasai pia waweze kuzingatia tamaduni ambazo hazina maana kwa wakati wetu wa sasa kwa sababu mnasema ya kwamba msichana anaweza olewa kwa boma nyingine. Lakini mkijaribu kuangalia maisha yanabadilika kana kwamba wakati huu wanaume hawapendelei kuoa, kwa hivyo unaweza kuwa na msichana pale na wewe unasema ataenda kurithi shamba katika familia ambapo ataolewa lakini utaona ya kwamba kutakuwa na wasichana wengi nyumbani kwa sababu wasichana ni wengi na wale wanaume wachache waliyoko hawataki kuoa. Kwa hivyo usipompatia huyo msichana urithi basi usingalimzaa kwa sababu ataendelea kuwa na shida kama hana urithi wa shamba ili aweze kujiendeleza kiuchumi.

Kwa hivyo ijapokuwa Katiba hii pia inazingatia mambo ya kuheshimu tamaduni za watu, ningependelea pia jamii ya Wamaasai

wajaribu pia kuzingatia vile maisha inabadilika na pendekezo kama hilo mlifikirie tena. Asanteni.

**George Nakholi:** Na nikiongezea tu kidogo, ukiangalia hii Constitution tuangalie kama Constitution ile tunaona itafanya miaka mia mbili inayokuja. Tusiangalie tu hapa mbele tu pekee yake. Kwa hivyo mambo inaenda kubadilika. Kwa hivyo tuangalie miaka 50, miaka 100 tuangalie itafanya na hii Constitution. Na ninafikiri ya kwamba Constitution itaandikwa kama sisi sote kwa hii room tumeshaenda. Labda watoto wa watoto wetu ndio watakuwepo.

**Alex Kipteng':** Kwa majini mimi ni Alex Kipteng', member wa NCCK Transmara. Mengi yamesemwa kuhusu mambo ya ardhi na machache yamesemwa kuhusu mambo ya watu kuheshimu *Inaudible*. Nilikuwa na pendekezo ya kwamba sisi kama wananchi wa clan ya Kimaasai, kwa sababu land yetu imezungukwa na hii communities zingine nilikuwa naomba pia ili commission nayo ipitishe sheria ya kuweza kuchunga boundaries zetu za Wamaasai ziwe zimechungwa kabisa.

Ya pili ni mambo kuhusu hii land leasing. Kama community inaweza kuelewana jamii ya the other party. I am talking now about the boundaries ya wale wengine, Wakisii maybe, wakikubaliana na hawa wajamii wengine ili waweze kuelewana vile wanaweza kutengeneza structure fulani ama sheria fulani ya kuweza kufanya leasing na isiwe ya muda wa miaka mbili na kuzidi mbili au tatu.

Jambo la mwisho ambalo tumesoma kwa hii draft kuhusu hii non-citizen. Mweka rasilmali anapewa miaka mingi sana. Hiyo miaka 999 hiyo ni mbaya sana mtu anakaa hata sisi tunakufa, watoto wetu watakuja tesa tena huyo mtu. Hiyo miaka tukae chini tuangalie ireduciwe irudi mpaka hata miaka 30 ama 20. Mimi nataka iwe 20 ndio pengine tufanye hiyo kazi vizuri. Asanteni sana.

**Maurice ole Raria:** Bwana Alex, nitarejelea kuanzia, tafadhalini hebu tuelewane. Bwana Alex ametoa mapendekezo tatu muhimu ana na ningependelea kurejea kutoka ya mwisho ya lease. Kusema kweli yale mapendekezo mnatoa hapa yametolewa Narok South na pia Kajiado katika sehemu zote na wananchi walikuwa wanaolea kwamba hata hizo miaka 99 ni nyingi sana. Kwa hivyo haikuwa jukumu letu kuwambia lease itakuwa ya miaka mingapi lakini tungependekea kusikia pia kama wananchi wa Transmara wanaona malalamishi yoyote kuhusu hii lease kwa sababu wananchi wa Kajiado walikuwa wanasema miaka 30, wengine wanasema nusu ya hiyo 99 tuseme miaka 45. Kwa hivyo hiyo tumenakili na mimi naona lazima tuwe na mabadiliko apo kwa sababu wanachi ambao wameathiriwa na mambo ya lease wanakubaliana juu ya kupunguza hiyo miaka.

Umesema pia juu ya lease baina yenu wananchi wa Transmara na majirani wenu kama vile Wakisii na kwamba pendekezo hili ningependa kuwaambia kwamba nimesema hapo awali kwamba ardhi yote itakuwa ya Wakenya na Wakenya wanaweza kumiliki mashamba lakini watu ambao ni non-citizens ndio wanaweza kufanya lease. Kwa hivyo watu katika hii nchi hawawezi kulease land bali wanaweza kumiliki kikamilifu either kwa njia ya kununua ama kuketi kama majamii. Kwa hivyo hiyo sheria ijapokuwa ni pendekezo lako na ni la makini ningependa kukukumbusha kwamba hapo awali nilikuwa nimesema ardhi yote ni

ya Wakenya na hawafanyi lease. Lease ni ya watu ambao sio wanakenya.

Pia kuna shida ya boundaries na ukisoma zaidi utakuta kwamba kuna commission ambayo itahusika na kujaribu kuweka boundaries na kuhakikisha ya kwamba boundaries zote zimeshughulikiwa ili kusiwe na shida ya land disputes ama mgogoro kuhusu mipaka. Kwa hivyo hayo mambo yameshughulikiwa na hii Katiba na pia pendekezo hilo lako nimeweza kunakili na litatolewa kwa commission.

**Daniel ole Tawasinga:** Mimi naitwa Daniel ole Tawasinga. Nilikuwa nimesema ninafanya na provincial administration. Mimi nimekuja kwa ajili ya lands. Kwanza kabisa mimi naenda kwa establishment of national lands commission. Ingawa mwenzangu ameongea lakini mimi nataka kuwajulisha ya kwamba, kwa kweli kabisa mlisema hii itakuwa Constitution ya watu wa Kenya, hii haitakuwa Constitution ya kule Nairobi tena. Mkipeleka hii inaitwa National Lands Commission, hiyo mmeanzisha kupatia watu nguvu tena ya kumiliki ardhi kule Nairobi.

Kwa hivyo mimi nasema hili jambo lirudishwe kwa wilaya ili tusikie shida yetu katika wilaya ya Transmara inafika wapi, kama tutatoa commission ya Transmara district. Kwa hivyo hiyo ya Nairobi msibadilishe but ile ya juzi iwekwe kwa jina lingine. Halafu mnasema pia ni parliament ndio itaenda kufanya hii. Hapana, parliament itaenda kufanya namna gani na sisi ni wachache? Wataenda kufinya sisi parliament? Sisi Wamaasai tuna wabunge saba ama ngapi? Sasa wale wengine wengi ambao ni wakubwa watafinya sisi, mahali wanamulika kwa macho mengi ni ardhi yetu, kutoka Kajiado mpaka Transmara na Samburu wanaangalia. Kwa hivyo mimi ninapendekeza ya kwamba watu wa wilaya waanzishe commission yao ya ardhi katika wilaya pekee yake. Hiyo inaenda hivyo.

Halafu mimi naenda kwa haya mambo ya ardhi kama ile ya kwetu, Maasai Mara. Kama Maasai Mara kama maji ya Indian Ocean ikipatiwa community, basi communities zingine Kenya zitaangamia mkikubalia zile communities ambazo zinaown maji itakuwa mnaanzisha ile serikali ile mnaita federal government ama Majimbo. Kwa hivyo hiyo haiwezekani. Tuwe na board kule juu ya kuangalia vile vitu ambavyo vinahusika na nchi nzima, national, maji, anga ya juu. Kwa sababu mimi nikimliki anga yangu na ndege ikipita juu nitakataa kabisa na mimi sina ndege. Kwa hivyo mambo hayo tuangalie kwamba, yaangaliwe vizuri. Constitution isiandikwe ambayo inatatanisha watu wa Kenya, na ni vizuri tuseme ukweli kwamba mambo mengine ambayo yaliandikwa, yaandikwe yale mambo ambavyo watu wa Kenya wanasema. Hiyo nafikiri ni land halafu classification hiyo ni mabarabara.

Hii heshima ya ardhi ambayo watu wengine wanataka kujua miaka ngapi wanataka kukaa, other communities wanataka kuweka miaka ngapi watakaa ndani ya ardhi ya wengine. Halafu kama watakaa na nguvu for more than 100 years si watachukua ardhi ya wengine? Hiyo mimi napinga. Nasema kwa wale watu ambao watakuja kwa utaratibu, mtu kama huyo ambaye atakuja kwa utaratibu vizuri, yeye akubaliwe na community, hiyo idepend na community. Isiwekwe sheria ya mtu ambaye anataka kukaa. Kwa sababu nilikuwa nasikia juzi juzi tu kortini kwa hivyo kortini insema 12 years ati mtu akikaa ana

qualify kuwa na shamba. Akikaa for 12 years tukipigana si atachukua shamba langu? Kwa hivyo tuchunge kwa sababu ardhi yetu iko nafasi na kila ndege ambayo inatembea juu hata nyinyi mmesema, Commissioners mmesema, mulikuwa mkipita na mabarabara hapo Transmara, Narok na Kajiado, mnaona ile kichaka kiko mnafikiri kinaitwa idle land. Ng'ombe wetu wanakula pale, boma zetu ziko ndani ya hicho kichaka. Hatuna nyumba ya mawe. Kwa hivyo kwa ufupi ninasema mambo ya miaka isiwekwe, community zikubali mtu mimi nikienda Trans Nzoia nikubaliwe na community ya huko. Thank you very much.

**Maurice ole Raria:** Jambo ambalo nilisema wakati nilikuwa nasema tafadhali tusikizane, nilisema kwamba kutakuwa na ardhi ambayo itaitwa public lands kwa sababu umesema kwamba kama kuna sehemu ama kusanyiko la maji kama vile bahari na ukisema kwamba community fulani ikimiliki italeta janga katika Taifa kwa sababu itakataza wengine rasili mali hiyo. Tulikuwa tumesema mambo kama maziwa makuu na sehemu kama mito hiyo itakuwa ni public haitakuwa ya community land. Nilisema kwamba mito na mabahari, kama Bahari ya Hindi nilisema hiyo ni public land. Kwa hivyo hiyo ni rasilimali ya uma kwa jumla sio community land.

Na pia umeguzia mambo ya Maasai Mara na umesema hiyo pia ni kama pia national resource. Na kama tungepata nafasi ili tuongee sana juu ya national resource vile Katiba imesema ni kwamba kuna hizi rasilmali ambazo zinapatikana katika sehemu ambazo jamii fulani zinaishi, na Katiba ilionelea ni vyema kama faida ambayo inatokana na hizo rasilmali iweze kufaidi wananchi wanaotoka sehemu hiyo. Sijui kama tunaelewana? Iwe kuna asilimia ambayo nyinyi mnaweza kupendekeza kwamba tunataka. Naam hiyo ni rasilmali ya kitaifa. Ni kweli, na inapazwa kufaidi Wakenya wote. Lakini kwamba Katiba hii inapea jukumu jamii kuweza kusema kwamba wanahitaji asilimia fulani ibaki katika hizo communities na kwamba percentage fulani iende katika national government. Kwa hivyo juu ya rasilimali hizo kama Maasai Mara pengine pendekezo ningependa kupeleka kwenye commission ni kusema ya kwamba kama rasilmali zingine ambazo zinapatikana katika jamii hii, mngependelea asilimia gani ibaki katika community na asilimia gani ya faida iende katika national government. Pengine hapo ndio tunaweza kuendelea vizuri. Kama kuna mtu ambaye anaweza kupendekeza kuwa wanahitaji kiasi fulani kibaki katika community na kiasi fulani kiende katika national government pengine hivyo tungependa kupata pendekezo kama hilo.

**Samwel ole Sankei:** Samwel ole Sankei. I wanted to summarize my views because I am rushing somewhere. Moja, juu ya hiyo percentage ya pengine Maasai Mara because that is a National resource and the communities are living there. My views are that 85 % of what is coming out of there must go to the community and then we give 15% to the national government. Pili ni swali kwa this land ownership. Mmesema ya kwamba what the council used to own, you want to tell us ile community sasa inaishi huku ndio itaown. We are asking that. According to me we must involve the community, which initially owned that land. I am just giving you an example. Tuko na shamba inaitwa Sosomael where I come from. Saa hizi iko under the council and in this neat Constitution ambayo tumetoa inasema the communities zenye zinaishi huku itakuwa yao. How, and yet sisi ndio tulikuwa original owners before we put it into the council? We have to be involved in the process ya kupea those communities which are living there. And in summary because I wanted to rush somewhere, let me summarize then I go.

We go to chapter four of this draft, page 12 part 2, number 2, 83 (2), it says the chairperson and other members of the commission shall be appointed by the president with the approval of the National Assembly. According to me, for example the next government, we don't know if it is the

Opposition and obviously it will have the majority in parliament. They will influence the Electoral Commission. Let me summarize. I am saying the election of the Electoral Commission should be to the political parties and not president it is depending on the strength of the seats of thel party in parliament. Like the one which is now there. Because the majority in parliament will win all the commission and they just rig the election.

We go to page 16 – 116 number 5, it says the deputy speaker shall be the chairman of all committees of the whole house. According to me the deputy speaker will be over-burdened. For example we have a health committee, a committee dealing with health, education. We are just giving one person all those posts and yet there are allowances for those posts. That means the deputy speaker will be a very competitive post for people to corrupt for allowances. Parliament should give both chairmen to be separate not the deputy speaker.

You go to page 19, 151 – authority of the president, 3 (a) it says, in the process of the cabinet, the president may appoint commissions of inquiry or, I just want to specifically come to commissions of inquiry. In the current system we have had so many commissions using our funds and yet we are not finding the findings!. According to me, we must have an authority to be given those duties, which the commission will collate. What is the need of appointing a commission, collecting the views and keeping the views? It is useless. Yes, like the Akiwumi Commission for clashes, like the devil worshiping commission. We are not doing anything! We have to be given! Those are my views, thank you very much.

**Maurice ole Raria:** Asante kwa mapendekezo yako ya haraka kwa sababu unaenda mahali na jambo ambalo ningependa kuzungumzia ni juu ya ardhi umesema ya nusu mile na ukiangalia katika pendekezo la Katiba inasema ya kwamba ardhi hiyo itarudishiwa community baada ya kuchunguza na kuidentify the original owners kujua ni community gani ndio walikuwa wamilikaji wa halisi. Kwa hivyo haitakuwa tu nyinyi ndio mko nayo chukueni. La. Lazima kuwe na uchunguzi wa kujua ni kina nani wamilikaji halisi halafu ikipatikana hapo ndipo sehemu ya nusu mile itaweza kurudishiwa wamilikaji wa halali.

**Gideon ole Geto:** Nataka kuchangia sehemu ya ardhi. La kwanza ningeomba Wakenya wenzangu ya kwamba tunajadili yale ambayo yapo sio yale ambayo yanaitwa imaginary. Kwa mfano kwa hili pendekezo, ambalo linaitwa historical claims, ukweli Wamaasai inajulikana ya kwamba walitoka sehemu za upande Uasin Gishu ………… Na kati ya miaka hiyo mpaka sasa kuna Wakenya wengine ambao wameishi pale na wamestawisha pale mpaka wakati huu. Tukiaribu kujidanganya mawazo ya kwamba eti tuende tuangalie wale walikuwa upande wa kwanza halafu ijulikane kama itarudishiwa wenyewe, mimi naona hii italeta mambo mazito katika nchi hii. So kama nyinyi tume mungeangalia kwa makini sana muangalie yale maneno ambayo yako mbali tuende tuyafufue, sijui mahali tunaelekea. Ndipo tunasema ya kwamba kama ni Katiba tupatie nafasi nzuri tujadili tuiangalie kwa undani mpaka tujue ya kwamba hii inafaa. Kwa sababu ndugu zangu wale ni Wakenya na sisi ni Wakenya na

mahali pengine mmesema ya kwamba wakenya wako na hake kuishi mahali popote katika Jamhuri ya Kenya. Wale watu wako pale si wanasema they are Kenyans and they have all the rights to live there? So tujihdharishe.

Lakini maswali yangu ambayo pengine ndugu yangu bwana commissioner ulikuwa unaelewa wakati tulipoanza ulituambia hii process ya kupata land certificate tunataka irahisiswe na vile uliposema ya kwamba irahisishwe hujatuambia basi umekuja na proposal gani ya kwamba sasa kwa sababu huwa tunapata title deeds hapa kwa district headquaters kwa land registrar, sasa kwa kurahisisha tutapata kwa njia gani. Sasa mkitupatia kwa ujuu still bado hatuoni, tunataka tuone exactly mnarahisisha kwa njia gani. Pia mmeandika katika sehemu 235 (a) section 4, sub -section 7 katika hiyo proposal ya hiyo Katiba mpya ya kwamba tutakuweko na resettlement of the landless since independence. Wale ambao hawana mashamba hata wale ambao wako katika miji, hamujatuambia mtaresettle kwa njia gani na mtaweka wapi kwa sababu currently, nchi ya Kenya umesema ya kwamba no idle land. It there is no idle land how are you going to ressettle these people? We want Kenyans to know how are you going to resettle them, in which way and where? Kama ni ile public land ambayo tumesema it is government land pengine mwingine ambaye asije kutwist sheria fulani aseme mtaalam wa sheria ni ya kwamba hiyo Maasai Mara ambayo iko pale ndio tulimaanisha kuressettle wale wengine na ilhali hiyo land ni ya Wamaasai. Usipotii sheria ni ngumu, we are not experts of law. So nobody can interprete it in another way ambayo itatufanya tulose our rights. We want you before you leave here to tell us where and how.

Kitu kingine ambacho it is very important here in Transmara mmetuambia land is the source of clashes or skirmishes here in Transmara. And that is true na mulituambia kwamba in view of that mnataka ya kwamba ile land isije ikawa tena a contributor to those problems. How are you doing that? We want to know (*Inaudible)*, that this way the electoral commission has come out with a solution of a source of problem in Transmara. So before you leave this hall that is what we want also to know haow are you going to do it, because those are statements from your own introductory remarks.

Tulikuwa tumependekeza ya kwamba all title deeds ulieleza ya kwamba lakini hatujaweka lile but why don’t you revoke. That is strong word ambayo sisi Wakenya tutajua kwamba ile ardhi ambayo umepewa kwa njia isiyo halali, the title deed which has been possessed in regular ways is challengable. We want that thing challenged. What is wrong kwa mtu kuchallenge title deed yangu tuje hapa kortini au tuende pahali pengine popote. If the other person has the right what about kama hana right nitabaki na title yangu so I don’t see anything added up. So what I wanted to say all title deeds ile ambayo itapeanwa 1000, ile ambayo itapeanwa another 1000 years to come, iwe challengable.

Jambo lingine ni kwamba, national land commission. Sisi tunaona ya kwamba this is the same problem. You are just changing the existing names or the existing government function to other new names. Because already we have a commission ambao iko Nairobi ambayo inafanya kazi ya Nairobi na pengine wale commissioners ambayo appointed in that commission are not part and parcel and automatically they don’t what the problem of Transmara is. So that is why we are saying instead of saying National land commission, say District land commissions. Because district people will be conversant with the problems of land

in Transmara.

Finally, mme-empower parliament tena. Kabla hii commission kuwa appointed kuna views zilisemekana ya kwamba why can't we give parliament to see what to do because they are the representatives of the people and most of the people of Kenya said no, those are just few people. And now tumeenda tumecollect pahali pengine ambapo maybe ni the center of everything. Tunakuja tena kuchukua pale na we refer again to parliament. The same parliament wataenda kuleta tena the same things ambazo maybe will contrary to certain individuals kushinda vile tungefanya we thought hii Constitution ingekuwa. Hapana wacha tena, eti kusema this Tunge expect mseme if the parliament haijasatisfy vile Constitution inasema we have the supreme court ambapo tunaenda pale na kuchallenge parliament if my rights are being threatened So I think those few remarks and I hope there are some other chapters which we are going to redo but still we request for you to give us time. Thank you very much.

**Maurice ole Raria:** Gideon ole Geto. You are talking from a very informed position na hii ndio sababu kulikuwa na pendekezo kwamba wananchi wangepatiwa muda mrefu wa kusoma hii Katiba kwa sababu ndipo tu wataweza kutoa maoni yao. Na hasa shida ya kutoa Katiba hii ama kuleta kikao kama hiki kwa muda ulio mfupi, unajua bunge ilipitisha tena sheria kwa sababu wananchi walikuwa wapewe muda wa siku 60, wasome hiyo Katiba ndio kikao kama hiki kikuje katika constitutencies lakini sheria ilibadilishwa katika bunge basi muda mfupi ukatolewa. Kwa hivyo tukiona wananchi ambao wanatoa maoni ambayo ni ya kiundani sana tunafurahia sana kwa sababu tunaona ya kwamba Katiba hii imevutia wananchi na inasomwa kwa umakini.

Ningependa tu kuanzia kuhusu mtu mwingine hapo awali alikuwa amezungumzia mambo kwamba bunge lisipatiwe tena jukumu la kuenda kupitisha sheria kuhusu ardhi na kwamba kungekuwa na pendekezo katika sheria kwamba, katika Katiba kwamba iwapo bunge halitaweza kusuluhisha hizo shida za ardhi baada ya muda ambao umepewa basi wananchi waweze kupeleka malalamishi yao katika korti ya juu sana ama supreme court. Mtu alikuwa ametoa pendekezo hilo hapo awali na tulisema ya kwamba ikiwa una pendekezo lililotolewa na mlifuria basi tusirudie kwa sababu tutakuwa tunarudi nyuma. Lakini ningependa kukuambia hilo pendekezo nimenakili tena na bila shaka tutapeleka katika commission.

Juu ya national land commission kuwa kule juu na kwamba haiguzii maneno yenu ya undani bali ni commission ya Nairobi, wananchi katika sehemu zingine pia wamesema hivo na pendekezo la district land commission sisi hatulisikii kwa mara ya kwanza katika kikao hiki, wananchi wenzenu katika wilaya ya Kajiado pia wamezungumzia hiyo na tumerecord.

Pia kipengele ambacho umelalamikia kusema ya kwamba inapaswa kuwekwa katika Katiba kuhusu kuweza kupinga mapendekezo ya umilikaji ama kuweza kuwa title deed ni challengable, na nilisema ya kwamba hakuna kipengele kimewekwa na umezidi kusisitiza ya kwamba kuna shida gani kuweka kipengele hicho katika Katiba. Basi tutatoa hilo pendekezo kusema ya kwamba wananchi wamesema ya kwamba hilo pendekezo walilotoa ya kwamba kuwe na kipengele katika Katiba ili kuonyesha ya kwamba waweza kuchallenge title deed, tutahakikisha ya kwamba hiyo tumefikisha katika commission na

kuwambia ya kwamba wananchi wamesema hatutaki maneno mengine kutumiwa tunataka kuona hiyo challengable kwa sababu ni neno ambalo liko na uzito. Kwa hivyo bila shaka hayo maoni tumechukulia kwa uzito sana na tutapendekeza kwa commission.

Tumesema ya kwamba commission imezungumzia juu ya mambo ya kusuluhisha mizozo ya ardhi na kwamba Katiba hii haijatoa suluhisho lolote na tumesema ya kwamba Katiba hii haingeweza kunakili kila kitu kwa sababu kama tungeweza kuweka katika Katiba hii, shida zote ambazo wananchi walizitoa hata jumba la mkutano la KICC, halingeweza kutosheleza shida hizo ambazo wananchi wametoa. Kwa hivyo tunasema ya kwamba kuna mambo mengine ambayo,majibu ya maswali yenu yote hayawezi kupatikana katika hii Katiba. na Kwa kusema ukweli kama ungekuwa na nafasi ya kusoma Katiba zingine za nchi zingine hayo maswali mengi ambayo wananchi wako nayo hayawezi kunakiliwa katika Katiba kwa sababu hii ni framework , structure, ambayo tu inaonyesha wananchi sehemu ya kupitia. Ni kuwaonyesha tu njia. Kwa hivyo mambo mengine ambayo hayajazungumziwa ama hayapewa undani katika Katiba hii yatazungumziwa katika sera za serikali yaani katika policy. Sera zingine ambazo hamjakuta hapa zitazungumziwa katika policy issues, na maneno mengine ama shida zingine.

**Speaker:** Yote ni kuhusu shida ambazo mmetoa, na kwa hivyo jambo kama hilo nimenakili na bila shaka litazungumziwa na ma-commissioner wakati watakutana tarehe ishirini na nane ili kama kunaweza na kuwa suluhisho ambalo linaweza kuwekwa kwa Katiba ijapokuwa najua Katiba haiwezi kubadili kila. Kitu lakini pendekezo hili mimi ninanakili kulingana na mapendekezo ambayo Katiba imetoa ama kazi ambayo walitupatia tukiwa hapa, kuwasikiza maoni yenu na kuyanakili na kuwapelekea vile wananchi wamesema.

Tumesema pia Katiba imezungumzia tu juu ya kwamba itarahisisha mambo ya title deed ama kibali cha kumiliki mashamba na kwamba Katiba hii hata haijaguzia ni vipi na ningependa kukujibu ya kwamba jambo hili litarahisishwa kwa sababu hivi punde tutaenda katika usambazaji wa utawala ama devolution na kwamba kutakuwa na serikali ya kijiji, tutakuwa na village councils na baadhi ya mambo ambayo village council inaenda kuzungumzia ni kwamba title deed yako hautakuwa ukihitaji kwenda kwa province bali utaenda kwa ofisi ya village council na mambo hayo ya title deed ama hata shida kuhusu ardhi katika sehemu ya kijiji, mambo hayo yote pamoja na title deed itaweza kupatikana katika village council. Kwa hivyo hiyo ndio suluhisho naweza kukuambia kwa sababu mmesema tunazungumzia tu juu ya mambo ya kurahisisha upataji wa title deed na Katiba haijaonyesha ni vipi, basi nakuambia kwamba tutakuwa na village Government katika kijiji chenu ambayo mtaona kwa kirefu hivi punde ya kwamba village government inaweza kusuluhisha shida hizo kama za title deed na mizozo mengine kuhusu ardhi.

Tumeongea pia juu ya historical reclaims na tumesema ya kwamba tukirejelea mambo hayo itakuwa ni kama opening of old wounds, kwamba kurejelea mambo hayo ya historia kunaweza tena kuleta kutatanisha. Na kwamba hayo ndio mambo yenye nilikuwa nimesema ya kwamba mambo ya legislation ama bunge wakikaa na wakiona wataona njia ambayo inafaa kusuluhisha shida hizo kwa sababu tukisema Nairobi sasa ilivyo ilikuwa ni nchi ya Maasai na kusema ya kwamba hiyo historical claim ikiangaliwa na watambue ya kwamba kumbe wenyeji halisi wa sehemu ya Nairobi ni Wamaasai, haitakuwa reasonable,

haitakuwa ni haki kwenda kubomoa jumba la KICC na hata kubomoa bunge ili Wamaasai waende wapeleke boma zao za ng' ombe pale. Kwa hivyo haya mambo ya historical claims hayatafanywa tu juu juu eti kusema kwa sababu nyinyi ndio mlikuwa hapa, hebu mtoke hapa mrudi kule. Ni lazima kuwe na mpangilio na suluhisho la kudumu ambalo ndilo tunasema bunge litaweza kurejelea mambo haya na kuhakikisha ya kwamba kutakuwa na suluhisho la kudumu kuhusu ardhi. Kwa hivyo mambo pia hayo ya historical claims tusichukulie juu juu ya kwamba wakaaji wenyeji watakapotambuliwa basi wataitwa waende watoe watu wanaoishi hapo ama wafukuzwe na wenyeji wa halisi waletwe pale.

Kwa hivyo ilikuwa tu napendendelea kurejelea mambo hayo, ili tuweze kuenda katika…….

**Ng'eno:** Nataka kuongeza juu, tunaenda haraka haraka kwa sababu saa imeenda sana. La kwanza kabisa ningependelea labda kuguzia juu ya watu ambao hawana ardhi, landless people. Kwangu kabisa ningeonelea kama serikali inajali maslahi ya Wakenya wote, iangalie sana maneno ya landless people, watu ambao hawana ardhi, ikifikia percentage fulani kwa sababu we cannot solve all problems and we cannot make the whole country mpaka watu wote wakuwe na ardhi. Lakini tupate kuona ya kwamba wale hawana ardhi kwa sababu fulani na ikifikia percentage fulani watafutiwe mahali pa kupewa ardhi angaa hata pa kuweka mifugo wao, especially from areas whereby watu wanamiliki ardhi kubwa na kwa njia ambayo wananchi hawajui. Na it is a situation in those Molo areas whereby watu walinunua ama walichukua ardhi ya ADC ambazo zilikuwa za serikali na wakajipea wenyewe, bila hata kuuliza wananchi wenye wangefaa warudishiwe. Kwa hivyo ningeonelea serikali iangalie sana mambo ya landless people ikifikia angalua 10% of the landless people in Kenya wakatafutiwe mahali pa ku-settle, so that they cannot have land problems any more.

Pia ningependa kugusia juu ya hilo swala ambalo limesema ya kwamba parliament after two years ……………..(Inaudible) to review the historical boundaries for the existing …………..(Inaudible). Well, hiyo problem haswa inaguzia sana Coast province, North Eastern province na Rift Valley, na inaguzia watu wengi sana. Na vile tunaona hata sisi, there is a serious problem affecting land and that problem was not created by Kenyans, it was created by the colonialists, the British who came to Kenya and evacuated the people who were existing in those areas to some other areas, halafu baadaye watu wanaende kukosa mashamba, wanataka kurudi mahali walipokuwa. Such problems have been cited in areas like Israel and so many others. Kwa hivyo ningeonelea bunge ijitahidi sana jinsi ya kufanya serikali ya Britain pay or to pay back all those people who were evacuated from their areas rather than to return them back to those areas.

Kwa hivyo serikali itafute mbinu ya kuongea na serikali ya Britain, ile ya Uingereza kuwalipa wale wale watu ambao walitolewa. Kama sisi wengine tulitolewa those areas Molo, tukatolewa those other areas in Kericho sasa watu wamepanda machai, na wa Wamaasai na hao wengine walitolewa huko Eldoret na sasa watu wameishi huko ni wa…………(Inaudible) tofauti sana. So, I prefer not to return the people to where they came from but the British Government should repay the people who were evacuated from those areas.

**Speaker:** Compensate.

**Ng'eno:** To compensate yeah, to compensate those people who were evacuated from those areas. Pia ili kutoa ile hali ya kutatanisha kwa sababu we can create tribal animosity should we say now, let us refer to the boundaries which were created by the Koitalel Samoei and the British or the Lenana and the British, such boundaries state that same areas belong to such people. Kama ya……………..(Inaudible) almost half of the Rift Valley belongs to the Kalenjins, tukitaka kuamua saa hii kuwatoa wale wale watu ambao sio Wakalenjin ambao wako nusu ya Rift Valley, wataenda wapi? The same case with the Maasais, tunajua they are almost being extinguished, they are a very small community. So tukisema nao pia ile mahali Lenana na wenzake walikuwa wamesema ni yao hao watu wote watolewe kutakuwa na ………………(Inaudible). So tunapendelea serikali iangalie ya kwamba the remaining areas ambazo sasa watu wanakaa should not be .………..(Inaudible) na watu wasiruhusiwe kuingia huko bila kuuliza wanakamati wa areas hizo. So we should create a situation whereby the land owners of that particular area have the power over the intruders in those particular areas.

Last but not least, ………………(Inaudible) kuguzia sheria ambayo inahusu watu ambao wamelalamika sana kwamba …………..(Inaudible) hapa……….(Inaudible). Well there are some agreements which were also made between the Maasai community and the Kipsigis community who are now……….inaudible). So those argreement pia lazima ziangaliwe ili isitokee a situation whereby the existence of a certain community is threatened with ………..(Inaudible). Kwa hivyo ningeonelea pia kwa Katiba hii i-respect as much as we would like to respect the ownership of the owners of these lands should also respect the agreement reached by the existing tribes in such a district. Kwa hivyo ningeonelea sana serikali iangalie mambo ya assent ambayo watu wengine walipewa and yet their situation in their stay here is being threatened.

Ya mwisho is the devolution of resources: Tukiwa na situation kama Maasai Mara, tuko na Maasai Mara ambayo watu wachache wameamua kutumia areas hizo kujipatia pesa, tungeonelea the titles of those particular areas should remain with the community who gave out or ambao wangefaa kuishi huko kwa sababu hii Maasai Mara huwa na watu ambao ………..(Inaudible) lakini kwa sababu ya wanyama wakatolewa sasa hiyo ardhi imekuwa ya wanyama. Tungependelea sana 70% ya hayo mapato ya huko Maasai Mara ipewe hao wananchi ambao wamekuwa wakiitisha ng'ombe wao halafu…………….(Inaudible) watoto wao hiyo ardhi.

Halafu the remaining 20% should be distributed to the whole district sasa kwa sababu kuna watu ambao wanaishi labda kwa ……….(Inaudible) na ardhi yao……..(Inaudible) huko Maasai Mara na hao wapate pia mapato ya huko. Watu kama wa Kipsigis nao pia wapate huko. Halafu the remaining 10% ndio iende serikali, why should the Government own almost everything, while the owners of that land own very little? Thank you.

**Maurice Ole Raria:** Asante Bwana Ng'eno, asante kwa maoni yako. Na hii issue ya resettlement ya squatters ama juu ya wale watu ambao hawana ardhi ni kwamba serikali itafute mbinu ya kuwapatia ardhi. Tumesema ukiangalia katika Katiba

ukiangalia kwa makini sana serikali, nasema kwa sababu kulikuwa na pendekezo hapo awali kwamba eti hakuna ardhi sasa Kenya kwa hivyo hawa watu hawawezi kupata ardhi, lakini ukisoma kwa makini sana, inasema ya kwamba kuna uwezekano wa serikali kutoa fedha kwa hawa watu ambao hawana ardhi ili waweze kuenda katika communities ambao wako na ardhi na waombe kama inawezekana wanunue. Kwa hivyo iwapo watapata fedha hizo kutoka kwa serikali kama serikali haina shamba za ziada kuwapatia hao watu, basi watapewa fedha watapewa pesa na wataweza kwenda mahali ambapo wanaweza pata ardhi na wataweza kununua na kuishi pale.

Pia hilo pendekezo ya kwamba lazima kuwe na compensation ama fidia na serikali ya wakoloni ama Britain ambayo iliweza kuchukua ardhi kutoka kwa communities za nchi hii, nimenakili habari hizo na bila shaka nitapeleka katika commission ili waweze kuona kama kuna uwezekano wa kushawishi serikali iweze kuwasiliana na serikali ya Britain kama inaweza kulipa wananchi ambao walipokonywa ardhi yao kama kuna uwezekano wa kulipwa fidia ama compensation. Mambo kama hayo ndio yatazungumziwa na commissioners na kwa hivyo hayo mambo yote tumeweka katika rekodi zetu.

**Philemon:** Naweza kuchangia, kwa jina naitwa Philemon ……..(Inaudible). Niko na mapendekezo kadhaa ambayo ningependa kuchangia siku ya leo, maneno ya watu kuitwa landless si nzuri, kwa sababu hata Wamaasai bado wako landless wengi, kwa sababu juzi hata mtu alifariki na kukosekana mahali pa kuzikwa kwa sababu hawana ardhi. Na ni kwa sababu walikuwa wanaishi huko na hii njia forest, katika Western Kenya ama sehemu ya Rift Valley pia Uasin-Gishu na sehemu hii ya Lugari, alikuwa anaishi lakini akatolewa.

Maneno ya landless watu wanaamini ya kwamba Wamaasai ndio wako na ardhi lakini wengi hawana. Ningependa tu kusema ya kwamba ambayo sitarudia Katiba iweze kuangalia isitoe kama vile nchi inaitwa Indonesia kwa sababu ilitoa kwa populated area, kupeleka watu sehemu ambayo inaitwa less populated na inaleta shida. Kwa hivyo muangalie jambo kama hilo lisitokee.

Jambo lingine maneno ya community hii ardhi ambayo iko kwa community, community nayo wana haki ya kuitumia na kufanya kwa sababu kwa jina inaitwa community kama group ranches lakini mtu mmoja anauza ardhi ya wengine kwa sababu yeye mwenyewe ameerevuka na anauza. Tuweze kuangalia jambo kama hilo zaidi kwa makini.

Jambo lingine ni hii land. Najua Kenya ni nchi kubwa na inatakikana chakula na bado inatakikana mahali ambapo watu watasomea na tusipochunga hii maneno kusema landless kila mtu apate, lazima kuna land ambayo itabaki katika Kenya iweze kutumika katika ukulima tupate chakula, kama ADC ili iweke maslahi ya taifa yaangaliwe sana. Kwa sababu pengine tutaweza fanya tukae tukae kila mtu achukue hekari moja moja katika sehemu ingine tofauti kutakuwa na watu ambao hatuna land ambao tutaitumia. Kwa hivyo mchungeze hii maneno ya ADC iweze kurudishwa na ingine katika kila mahali ili yaangaliwe kwa maneno kama hayo. Kwa sababu ukiona kama nchi inaitwa Netherlands, ni nchi ambayo watu wamejaa lakini wana mbinu, wana ardhi ambayo wamebakisha ili watumie katika maendeleo ya taifa, na hata vile vile China, Israel na nchi zingine ambazo wanaangalia maslahi ya taifa lao.

Kuna hii maneno tulisema ya colonial agreement, iweze kuangaliwa vizuri sana, siwezi kurudia kwa sababu wengine wameshasema.

Jambo au mambo ya registration act hiyo mtu anaweza register tu na haangalii tu mambo kama hayo, katika Transmara tulikuwa na shida. Baba wakati alikuwa anaandikisha shamba lake, anaandisha kijana wa kwanza vijana wanaongezeka. Na sheria inasema yule aliyeandikishwa ndiye mwenye haki. Sasa Mzee anakaa kama miaka kumi, Mzee anagawa na vijana na hapo……….(Inaudible). Sasa hao wataenda wapi? Haya maneno ya registration yaweze kuangaliwa kwa makini sana ili kila mtu atakaye andikishwa kila ukizaa mtoto waweze kuandikishwa tu hawa nao wawe na hiyo haki ya kupata hiyo ardhi.

Halafu kulikuwa na magendo mengine yalikuwa yanafanyika kwa sababu shamba letu ama shamba la wazee, ilikuwa ni wakati watu walikuwa hawajaerevuka. Mtu mwingine kutoka mbali anajitenga anaandikisha na hiyo shamba ama Mzee kama hawezi kuwa na, kwa sababu ya ardhi inasemekana yule haliyeajiriwa atakuwa na haki na wakati mwingine hawakusoma. Taabu hii imeingia katika sehemu hii ya Wamaasai. Asante.

Jambo la kuuza ardhi mimi ningependeza kwamba ardhi isiuzwe katika area hii ya Wamaasai. Utasikia wale maskini sana katika Trans-Mara ni wale waliuza ardhi, hiyo ndio ililetea Wamaasai umaskini na hilo jambo la ardhi liweze kutupiliwa mbali. Na ningependekeza kitu kimoja, hiyo na lease: mtu wa lease miaka ishirini na isipite miaka hamsini ili kumaliza hii maneno ya kusema kuuza ardhi, hiyo ni lease sio kuuza ardhi. Kwa hivyo Katiba iweze kuchunguza, hakuna kuuza ardhi hata Mungu naye alisema katika Bibilia kwamba ardhi isiuzwe.

Jambo lingine tunataka tuangalie mtu anaruhusiwa kuuza ardhi kiasi gani katika nchi hii ya Wamaasai. Anauza ardhi kwa nini? Kwa nini anauza ardhi, community ijue kulingana na ile council vile mli……..(Inaudible) kwa nini anauza ardhi. Mtu anaweza kuuza ndio aende mastarehe. Kwa hivyo tunataka tuangalie kwa nini na mtu akiuza ardhi tafadhali asiuze zaidi ya eka tano, kwa sababu hiyo inaweza kuwa amekula na hakuna vibaraka hakuna jambo……….(Inaudible).

Jambo lingine la mwisho ni kwa sababu kuna hii maneno ya boundary, ningependa kusema hivi, iweze kuheshimiwa Katiba haiwezi kueleza iheshimiwe. Na maneno itamaliza hii yote, Katiba ikitafuta namna ambayo tunaweza angalia mbele sijui lakini maneno ya corruption, mnajua corruption ikiisha maneno mengi, mengine mengi yatakuwa mpaka wewe unashangaa. Ninapomalizia watu………………..(Inaudible) namna ya kutumia ile ardhi. Mnajua kama ile nini ilikuwa inasemakana ya Zimbabwe anapatia watu ardhi lakini hawezi kujimudu kujisaidia. Kwa hivyo Katiba iweze kuangalia ipatie wananchi kitu angalau kitu kidogo katika sehemu hii tuliwachwa nyuma sijui kwa nini, lakini ili watu waweze kutumia ile ardhi kwa njia inayofaa.

Halafu kuna hii …………….(Inaudible) na hii ma-loans imetuweka shida. Mtu anaenda kwa groups branches wanakamati wawili ama waende kamati kumi na tatu au kiwango hiki, wanaweza kushika loan kwa shamba hata wenyewe hawajui, inaenda

group ranch iko na deni, na kwake ana deni kweli na ……………(Inaudible) si wapate wizi?

Jambo lingine hii community iweze kuangaliwa, mimi mwenyewe kama mimi naweza kweli kupatiana shamba la wenyewe kwa niamba ya wengine? Kufanya hivyo kwa niaba ya wengine hiyo ndio inatuletea shida. Kwa hivyo ikifikiwa miaka hamsini mtu hawezi kudai ile haki yake hawezi kujidai kulingana kwa sababu hiyo imetuletea shida mingi…………………………….(Inaudible).

**Maurice Ole Raria:** Ni muhimu sana hasa ukizungumza juu ya uuzaji wa community land, kama ulikuwa hapa hapo awali nilipokuwa nikizungumzia juu ya community land, nilisema ya kwamba kutakuwa na sheria, sheria kali sana ili ardhi ya jamii kama hizo umesema group ranches watu wasiwe wanakaa pale kama officials halafu waweze kuuza community land, niliongea juu ya hiyo nikasema ya kwamba kutakuwa na sheria kali ili kulinda ardhi ya community.

Na pia nilisema hata wale watu ambao wako na title deed lazima pia kuwe na sheria kuhakikisha ya kwamba hawatakuwa wanauza mashamba yao bila sababu yoyote. Kwa sababu tutakuwa na serikali katika kijiji lazima wawe wakiketi ikiwa unataka kuuza ardhi ni lazima uende katika ofisi zifaazo halafu uweze kuwaeleza kinagaubaga ni kwa sababu gani unataka kuuza ardhi. Kwa sababu imeonekana kulikuwa na uuzaji wa ardhi wa siri ambapo mnaenda kuelewana kando kando na mtu fulani mnauziana ardhi halafu hadi umalize ardhi yote na unawachia jamii mzima shida, kwa sababu lazima uko na watu wa jamii yako na wakati huo utamaliza ardhi yako hiyo shida ya watoto, hali ya kuwalisha utarudi kwa jamii hizo. Kwa hivyo hata ukiwa na title deed kutakuwa na sheria kali ili kukataza uuzaji wa ardhi bila sababu yoyote. Kwa hivyo asante sana kwa mapendekezo yako, ni ya muhimu sana nafikiri kwa watu wote walio hapa na hata wengine ambao watakuja kuona mapendekezo kama hayo katika ile Katiba ya kesho.

**Said:** ……………………..(Inaudible) tuko na Programme Officers na …………..(Inaudible). Maoni yangu ni ………………(Inaudible) kwamba tumesikiza maneno ya ………………(Inaudible). Mimi naona ni kama ni taabu sana, tumeendeshwa haraka sana, ni taabu sana na tumesumbuka. Swali langu ni kwamba katika yale mapendekezo katika Katiba ya Kenya ambayo mlisema yatabadilishwa (?) mpaka sasa. Tumekuwa na ugumu mmoja kwamba mambo yanaandikwa kwa kitabu, mambo yanasomwa kwa kitabu cha sheria, yanafanywa nini, lakini kutekeleza, sidhani kama tumefikia pahali. Kwa sababu hii Constitution ya sasa vile vitu nimesoma, nimesoma nimeipitia hiyo draft mara mingi. Na mimi ninaona ni tamu sana na nimesoma hii (?) ile ambayo mnasema mnataka kubadilisha.

Swali langu ni kwamba kama (inaudible) vile tunavyoenda sasa (?) mpya, wale watu ambao wataenda kutekeleza tuseme kama maofisi, tuseme kama majudges, wale wako katika mahakama yote Kenya, na wale wenye kutengeneza sheria wengine wote ambao mnajua. Hawa wote ni wale ambao walikuwa huko jana, watakuwa leo na wanakuwa kesho. Wakati mtu anapoenda kubadilika, kama umeokoka, ulikuwa unafanya mambo mengine halafu tu ukasema umeokoka sasa unafuata maisha mengine mapya. Sasa swali langu ni kwamba, katika kutekeleza hii Katiba, tuna uhakika gani

kwamba kwa sababu mimi shida yangu ni kwamba hii kitu kimekimbishwa sana kimeenda haraka na kila watu wote wa Kenya wanasema ni tamu, ni mzuri kabisa. Sasa tukienda kumaliza kwa sababu tutaenda Constitutional Conference na watu wameshachaguliwa na wamekuwa gazetted itapitishwa. Sasa swali langu ni hili, ni hali ya kutekeleza, kwa sababu hii sheria …………….(Inaudible) nani anaenda kutekeleza na wale watu ambao walikuwa jana, leo na kesho ni wale wale. Una hakika gani kwamba haya maneno matamu yote ambayo tumesema yatatekelezwa namna gani?

**Maurice Ole Raria:** Asante kwa swali lako Bwana Said. Ni kwamba shida yako na hata ya Wakenya wengi pengine sio Wakenya wengi wamezungumzia jambo la utekelezaji kwa mapendekezo ya Katiba lakini ni vizuri umezungumzia juu ya hiyo, na umesema ya kwamba wale watu, wale wako hivi sasa ndio bado watakuwa hata katika Katiba mpya.

Na tukijaribu kuangalia kwa mambo ya utekelazaji, ikiwa umesoma kuhusu the judiciary ambao ndio hasa wanafanya mambo ya utekelezaji wa kazi ya Katiba ama mapendekezo yetu ya sheria. Wale wanaofanya utekelezaji ni majaji na ukiangalia kuna mapendekezo mengi ya wakati wa awamu ya mapito ama transition government. Lazima kuwa na pendekezo fulani kuhusu majaji kwa sababu tumesema lazima miaka ipunguzwe kutoka sabini na nne ambayo majaji wanahitimu ili waende retire. Katiba hii imebadilisha hadi miaka sitini na mitano, kuonyesha ya kwamba, wale ambao wako pale, na ambapo mnajua shida kubwa sana ambayo wananchi walizungumzia ni kuhusu sheria. Basi wale watakuwa hapo ambao kama wengi wao ni wazembe, hao kwanza lazima waende kama hii Katiba mpya itaweza kutekelezwa.

Na tumesema ya kwamba mapendekezo yako katika sheria hii. Tumesema katika haki za kimsingi, tunasema ya kwamba taifa ama serikali, wakati hii Katiba itakapotekelezwa, ni lazima kutekeleza majukumu ambayo yametolewa katika Constitution hii ama Katiba hii. Na kwamba iwapo serikali haiwezi kutekeleza majukumu haya ama kutimiza haki za kimsingi za wananchi, basi hiyo serikali haifai kuwa pale. Na vile unasema ya kwamba kutakuwa tu wale watu wako katika Katiba hii, ndio watakuwa katika Katiba mpya.

Na umesema ya kwamba huwa binadamu akisema ameokoka amekuwa kiumbe kipya, basi na sisi tunasema ya kwamba wale ambao wataweza kutekeleza Katiba hii mpya wale watakaoenda kuzingatia mapendekezo ya Katiba hii mpya watakuwa wameokoka. Tunasema ya kwamba iwapo wale ambao watakuwa katika nyadhifa mbali mbali za serikali ama watakuwa wakishikilia watakuwa wakishikilia nyadhifa mbali mbali katika maofisi ya serikali, na wafuate Katiba hii kwa umakini, basi itakuwa ni rahisi kutekeleza mambo hayo. Kwa sababu ukijaribu kuangalia haki za kimsingi, hazijaweza kutekelezwa katika Katiba tuliyo nayo hivi sasa. Ni kwa sababu haki za kimsingi hazijapewa umuhimu. Haki ya kimsingi kama chakula katika Katiba tuliyo nayo hivi sasa, haijazingatia kusema ya kwamba ni lazima kila Mkenya aweze kupata chakula. Na katika Katiba hii, inasema ya kwamba ni haki ya kila Mkenya, kuhakikisha ya kwamba au Katiba hii itahakikisha ya kwamba kila Mkenya ataweza kupata chakula. Na ikiwa wewe utakuwa na njaa, na ukifungua Katiba yako ukiifungua katika the promise ambayo umepatiwa katika haki ya kimsingi, wewe uko na njaa na unaona ni haki yako katika Katiba kushiba, una haki ya kuenda kortini na kusema ya kwamba mimi niko na njaa, na wewe jaji mimi ninaona huwa unaendesha Mercedes, na mimi niko na njaa

kwa hivyo ningependelea uuze gari yako ya Mercedes, ununue Peugeot kusudi kijiji chetu kiweze kupata angalao madebe kadha au magunia fulani ya chakula.

Kwa hivyo tunasema katika Katiba hii, tofauti ya hii na ile ya zamani ni kwamba kulingana na Katiba hii unaweza kumshtaki mtu katika korti ikiwa kuna haki yako ambayo umenyimwa, unaweza kuenda kortini. Lakini haki ambazo zimepewa katika Katiba tuliyo nayo sasa, hauwezi kuenda mahali, imepewa tu pale katika Katiba lakini hakuna njia ya kutekeleza. Kwa hivyo hiyo ndio tofauti kubwa sana katika Katiba ya sasa na Katiba mpya ambayo wananchi wameadimia itaundwa.

**George Nakholi**: Na nikiongezea tu hapo, hii inaweza kuwa nafasi zaidi na nzuri kabisa, nzuri kabisa. Lakini kama hakuna nia kwa wananchi wote, hakuna kitu mtafanya, hakuna kitu mtafanya. Tuseme upande wa corruption, tunakuwa na watu wawili; yule anapeana na yule anapokea. Sasa ni lazima, kama Wakenya, ni lazima tuwe kwa hali ile ilikuwa ya sole (inaudible). Hiyo ndio itatusaidia. Hii inaweza kuwa nzuri sana, tuseme (?) itakuwa vizuri sana, lakini sisi kama hatujabadilika tumefanya kazi bure.

Nafikiri kama hakuna kitu kingine sasa, twende kwa (inaudible) jambo hata unaweza kusema tu, very brief.

**Justus Owino**: Thank you very much Bwana Chairman. My name is Justus Owino Ouko. I am the (?) secretary, (inaudible). Nimesema I have got very few remarks made from our draft constitution. We would like that the government when making appointments, it should make clear that those appointed are promoted regularly as pertaining the (?) which are affordable (?).

After appointment, those appointed should be given tools to perform their duties effectively. For example, most of the resources in the government are going to waste. We have got the Extension Officer in the Agricultural Department. These people are deployed here and they are not given tools to perform their work which of course in the end it is a waste.

The scheme of service for those who are appointed. The government should make sure that the scheme of service which is enacted must be viable to enrich those who are employed. On remuneration, the government should make sure that all public servants are paid according to their academic qualifications. For example, here we have the Judiciary department, our main goal is to serve the government. These people are paid so much money, compared to others, why? And we are dissolving the current government, are they doing or giving us any special services? My dear friends, is it true? Why should they, are they, being bribed?

Training opportunities…Bwana Chairman, all those people who are employed by the government must be given the opportunity for training so that they get the chances of moving even up to the highest job groups. There is something which is now

happening in our civil service, these people (inaudible). Somebody may work under one job group for more than fifteen years. This is a person with children in schools, if he is not promoted, how will he manage to educate his children? That is still corruption, we don't want this.

Allowances; Bwana Chairman, the government should make sure all its employees are paid their allowances kulingana na their personal capabilities. We have got house allowance, we were told this in (inaudible). I just need to ask you a simple question; a subordinate staff who is a parent, my children he is rearing are Kenyans. She is staying home (?) where can you get a house to live with a family ……..(Inaudible)? Is it possible? So Bwana chairman in a few words this constitution makes sure that the lives and welfare of the civil servants are greatly taken care of.

Another thing is, this is another also where problems are, our friends teachers although they are now striking to be given some more money, here it has emerged teachers are being paid hardship allowance while …………..(Inaudible) and I am his senior secretary, …….(Inaudible) you are not being ……….(Inaudible) and we are serving the same man, the same area, the same………..(Inaudible) where is ……..(Inaudible).

So Bwana Chairman such things should not happen in the ………..(Inaudible) if this ………(Inaudible) of other workers. Retirement benefits, Bwana Chairman I am proposing that before a serving officer retires, before he leaves he must be paid his last dues promptly and I am urging if possible, you should not go home before you are paid that due. Because Bwana Chairman if I should define, there are so many brothers and sisters who have worked for this Government tirelessly, they go home, they wait for these last benefits, if they die that one will be another problem also.

Then Bwana chairman of late in the draft proposal, it is written that they want the new constitution to remove provincial administration department. Bwana chairman this one should not work, this one cannot work because these people they are the link between government and the people ………..(Inaudible). So if they are removed there will be a vacancy between the Government and the people. Although we know human beings are ……………(Inaudible) there are some DCs, PCs and DOs who have done wrong things, and chiefs, let everybody be taken as per what he has done but not ……………….(Inaudible). Bwana chairman I think I don't have much, I just ……..(Inaudible) from there, thank you very much.

**Speaker:** Sawa.

**Justus Owino:** It is okay.

**Maurice Ole Raria:** Jambo la mwisho umeongea ni juu ya utawala, about the provincial administration yaani utawala wa mikoa. Na ningetaka kukuambia kwamba jambo hili nitazungumzia kwa kirefu tukienda katika usambazaji wa utawala, ambapo

tutazungumzia juu ya administration baada ya maswali haya, kwa hivyo tutaweza kuzungumzia juu hilo jambo.

Mambo pia ya retirement benefits za public civil servants kuna report pia iko sambamba na hii constitution na nikianza tu kuwadokezea mapendekezo ya Katiba kuhusu retirement benefits, Katiba imesema ya kwamba ni lazima mfanyikazi wa serikali ili aweze kupata retirement benefits zake ikishikana pamoja na mshahara wake wa mwisho, tunaelewana? Siku ile unapata mshahara wako wa mwisho, pia upate retirement benefits, hiyo itakuwa ni option ya kwanza.

Option ya pili ni kwamba public civil service kama bado wanatayarisha retirement benefits zako, basi kwa wakati ule wanapotayarisha basi wewe uendelee ukae kazini ukipata mshahara hadi siku ile watamaliza.

Pia pendekezo la tatu kuhusu retirement benefits kama ilikuwa ni lazima uende retire ama ustaafu kwa sababu ya umri na huwezi kuendelea katika civil na hata kama ungependelea kukaa hapo ukingojea marupurupu yako, basi tuna pendekezo la tatu kusema ya kwamba na utaenda nyumba lakini muda ule wote ambao wanaendelea kutayarisha retirement benefits, basi itakuwa iki-accrue interest. Tunaelewana? Lazima kuwe na interest ambayo ile retirement benefits zako kabla hujapewa kama itabidi wewe uende ungojee retirement benefits kwa muda fulani basi iendelee kupata interest mpaka wakati ule utakuja kuletewa. Kwa sababu ikiwa utaenda nyumbani uketi na ile retirement benefit utaletewa ni ile ilikuwa ya mwaka uliopita basi maisha ya wakati huo itakuwa imeenda juu, kwa hivyo haitakuwa na faida. Basi tunasema ya kwamba lazima kuwe na generous interest ambayo utaendelea utapata na hiyo retirement benefits na wakati utaletewa haitakuwa ile ulikuwa supposed kupata wakati ulikuwa ………….(Inaudible) bali itakuwa zaidi ya hiyo.

Na tukienda sehemu ya national resources, utaenda kusoma juu katika chapter 14 ambayo imeongea juu ya the public service na utakuta ya kwamba kutakuwa na commission ya Public Service Commission na sio vile unaijua hivi sasa ni kwa sababu kunahitajika kuwe na uajibikaji. Na jambo la muhimu ambalo litahakikisha ni kwamba wafanyikazi wa serikali watakuwa na haki ya kupata mishahara kulingana na kazi zao, kwa sababu inaonekena ya kwamba hata ukiwa na qualifications za aina gani na unafanyia kazi Public Service hakuna mshahara ambao unalingana na ile kazi ambayo unafanya. Kwa hivyo ita…

Imetekelezwa katika commission hii kuhakikisha ya kwamba kutakuwa na tume ya kushughulikia mambo ya mishahara ya watu wote wa serikali ili kusiwe na mbunge ambaye anapata nusu milioni ya mshahara na wewe unapata ukiwa unafanyia kazi serikali unapata shilingi elfu tano, na ilhali ile duka unaenda kununua vifaa, sukari ni bei sawa, ukienda kununua utatumia shilingi hamsini na tano na yule Mheshimiwa Mbunge akienda pale kununua sukari hata yeye atalipa shilingi hamsini. Kwa hivyo tume hii ambayo imependekezwa na Katiba hii ni kuhakikisha ya kwamba kuna harmonization ya salaries. Kwa kusema kweli naam hatuwezi wote kupata mshahara uliosawa lakini lazima kuwe na kiwango fulani ambacho serikali itapitisha kuhakikisha wafanyi kazi wote wa serikali ni sharti yule anayelipwa ama mtu yeyote yule ambaye ako katika salaried employment kuwe na limit ya kwamba hakuna mtu yeyote anayefanya kazi katika sehemu yoyote, iwe ni private sector ama ni public service kutakuwa na kiwango ambacho mshahara hauwezi kushuka ili iwe mtu wa mwisho wa kulipwa kabisa inaweza semekana ni shilingi elfu kumi,

ili kulingana na ngazi zingine za job group waendelee kupata mishahara ambayo inafaa kulingana na kazi zao. Kwa hivyo juu ya public service mnaweza pia angalia hapo katika national resources kwa wakati wako na utaelewa. Asante.

**George Nakholi:**…………….(Inaudible) nikiongeza tu kitu kidogo hii ni ……………………………..(Inaudible) hapa, na yule afisa ambaye anachelewesha……(?) constitution na tuko na administration …………..(Inaudible) kwa sababu……………(Inaudible) violate hiyo constitution kuchelewesha ni very different……………………..(Inaudible). Asante.

…………………………(Inaudible) kutoka asubuhi nafikiri tumefanya kazi nzuri kwa sababu vile nilisema hilo ndilo jambo tulikuwa tumeona kwa hizi communities they are being …….(Inaudible) za hapa Trans-Mara, Narok na Kajiado. Hilo ndilo jambo liko na uzito sana, limemalizwa. Yale yanayobaki, yale hamjasoma hii sana mtaenda msome lakini tutaendelea kuangalia ili muende msome wenyewe na muangalie zaidi.

Sasa tutaangalia kwa ufupi sana juu ya executive power of President, wale wako na hizi pullout ni ukurasa wa kumi na tisa, angalia hapo tutaenda tu kwa haraka haraka ili kama kuna jambo ambalo huwezi kukuwa vizuri au kuelewa vizuri unaweza kusoma ukirudi nyumbani na tujadiliane kwa ufupi. Basi vile tumekuwa tunatembelea nchi tukienda kwa ma-constituencies kuchukua maoni, watu walikuwa wanalia sana juu ya power ya executive ama power za President. Walikuwa wanalia iko nyingi sana, sijui ana nini, ana nini, ana nini, lazima iwe chini. Na jambo hilo lilikuwa pia chini ya commission kuangalia ya kwamba kwa Katiba hii President awe na powers ambazo zinaweza kwenda kwa wananchi awe mfanyikazi wa wananchi sio ati ni mkubwa wao.

Kwa hivyo ukiangalia kwa ukurasa kumi na tisa utaona zile powers za President, mkiangalia hizi powers za President za executive kwa Katiba hii ni nyingi sana tunaita ceremonial powers. Hazijaenda zote lakini zile ziko ni zile kama za kuendeleza nchi, ambayo ndiyo msingi wa nchi, anaonyesha unity ya nchi yetu ya Kenya, hilo ni jambo moja la muhimu kabisa. Anafungua bunge na kufunga, hiyo ni kazi amepewa, hiyo ni kama ceremonial vile nilisema. Pia anaweza kutokana na ile kama bunge, bunge sasa vile mnajua tumekuwa hata sasa vile tunakaa hapa President kwa constitution iko anaweza kuvunja bunge saa yoyote, hiyo anapewa hizo powers na constitution ambayo iko. Lakini kwa constitution hii tunaona hapa bunge itakuwa na kalenda yake yenyewe, kwa sababu itakuwa na kalenda ya miaka tano, itafunguliwa lini, itafunga lini. Lakini President kama symbol ya unity na kule juu ndiye atakuwa anafanya hiyo kazi lakini sio ati anafanya kama vile anafanya saa hii, anafanya kama kazi tu ya kuendesha.

Sasa kazi ingine ya President ukiangalia kwa hiyo page, hiyo hiyo, kipengele mia moja hamsini na moja, mtaangalia na kuona ya kwamba anaweza, jambo kubwa alilo nalo ni kuteua Prime Minister lakini hafanyi hiyo pekee yake, lazima apate idhini kutoka kwa parliament, hilo ndilo jambo anafanya. Lazima apate idhini kutoka kwa parliament ndiyo ateue Prime Minister. Nitakuja kusema juu ya Prime Minister pia.

Anaweza ku-appoint High Commissioners na Ambassadors, hiyo ni kazi yake na anaweza pia kupokea Ambassadors, na watu wengine mashuhuri wakija hapa Kenya, hiyo ni kazi yake. Pia anapata habari kutoka kwa advisory council ambayo itakuwa juu sana kuongeza juu ya Supreme Court kama ile itakuja tukienda kwa judiciary na mambo yote atakuwa anachukua kutoka hapa chini kwa cabinet na parliament. Pia atakuwa na lile jambo, kama wewe umefanya makosa kama labda umefanya kosa na President anaona anaweza kukupatia msamaha anaweza kufanya hivyo, hiyo ni kazi anafanya. Lakini anafanya hii yote akiwa na consultation na Prime Minister au wanabunge.

Anaweza pia kuwa na jambo la kufanya, lazima tuseme kama anaona hii nchi, nawapatia tu mfano, anasema hii nchi nataka iende kwa vita, hawezi kuchukua hilo jambo pekee yake; lazima atajulisha bunge na bunge lijadiliane ndio lipitishe au limwambie hapana, na hawezi kuendelea kama bunge limekataa.

Sasa tuangalie kwa ufupi huyu President atakuwa mtu wa aina gani. President atakuwa akichaguliwa na nchi nzima, hatakuwa na constituency ati President huyo constituency yake ni Trans-Mara hapana. Atakuwa wa nchi yote, constituency yake itakuwa Kenya. Na atakuwa anatoka kwa ile party ambayo hatakuwa na party lakini atakuwa anachukua Prime Minister kutoka kwa ile party ambayo………(Inaudible) iko na ukubwa, iko na watu wengi kwa parliament. Kwa hivyo yeye na Vice President wake watakuwa watu ambao hawapigiwi kura na constituency kama Trans-Mara au kama Narok South, atakuwa mtu anapigiwa kura na watu wote wa Kenya ambao wako juu ya miaka kumi na nane.

Atakuwa mtu wa miaka thelathini na tano kufika sabini, hapana juu ya hiyo thirty five to seventy years. Atakuwa mtu ambaye yuko na degree kutoka kwa chuo kikuu kinachotambulikana, recognized University. Atakuwa mtu ambaye ana ile moral behavior au yule watu wanamwangalia kama huyu mtu ni mtu wa haki, si mtu yuko na mambo ambayo watu watasema huyu yuko namna hivi, ni criminal au nini, hapana, mtu ambaye yuko straight forward atakuwa hivyo.

Atakuwa mtu ambaye kwa watu wa Kenya anasimama mbele ya watu wa Kenya kama symbol of unity, kwa hivyo ni mtu ambaye atakuwa namna hivyo.

Vice President wake atakuwa yeye ndiye anamchukua anasema huyu ni my running mate, huyu ndiye nitakuwa na yeye kwa kuwa Vice President na huyo pia ndiye ataenda na yeye. Hakuna kura kwa Vice President, yule amemchagua ataenda naye na atakuwa ndiye akishaingia kama amepigiwa kura na Wakenya wote, huyo pia ataingia kama Vice President wake. Hapo ndio jambo la executive.

Sasa term yake ya President itakuwa miaka mitano kwanza na tena akipigiwa kura atakuwa na miaka mitano mingine, kwa hivyo miaka kumi, hiyo imetosha. Maximum of two terms of five years each, na tena hivyo kwa Vice President.

Kwa hii constitution Vice President anakuwa assistant wake, jambo lolote likifanyika kama yeye yuko nje ya nchi Vice

President anaingilia kushikilia hicho kiti cha President. Vile vile bahati mbaya akifariki, Vice President atachukua mahali hapo, kwa hivyo huyu ndiye executive assistant wake, direct.

Sasa tukiangalia kwa hiyo kuna mambo mengi inasemekana nilikuwa ninasema, hii mtasoma baadaye muangalie. Kwa yale mambo mengine kama Prime Minister ukiangalia ukurasa ishirini na moja, hayo mambo ya mshahara na allowances na nini Bwana Ole Raria alikuwa amezungumza, na ile commission inaitwa Salaries and Remuneration Commission. Hiyo ndio itaangalia mishahara ya watu kama President na Vice President.

Sasa huyu Prime Minister ndiye mtu ana mambo mengi kwa constitution, kwa sababu ndiye anaendesha serikali day to day. Na constitution hii inapeana sasa tuwe na Prime Minister, halafu tuwe na two Deputy Prime Ministers. Prime Minister huyu, na hapa muangalie vizuri sana, Prime Minister huyu anatoka kwa chama ambacho kiko na wabunge majority parliament, na chini yake tutakuwa na two Deputy Prime Ministers na Waziri au Ministers kumi na tano, wasizidi kumi na tano, maximum is 15 Ministers na hawa Ministers watatoka nje ya bunge. Sasa hawa ni professionals, hakuna mambo ya Army General kuwa sasa Minister wa afya, hiyo imeenda, hakuna sasa. Sasa Minister anaingia kama professional akiwa Waziri wa afya atakuwa daktari, akiwa Waziri wa elimu atakuwa anajua mambo ya elimu. Mtu wa mifugo atakuwa mtu amesomea hayo mambo. Sasa hayo ndio itakuwa kwa hii Katiba na huyu Prime Minister atatoka kwa kile chama ambacho kina ukubwa kwa parliament na parliament yote ndiyo inaangalia kutokana na vile wanapiga kura.

Ikiwa parliament inampitisha wanapeleka kwa President, wana-nominate halafu wanapeleka kwa President for appointment. Sasa parliament ina jawabu kubwa la kuchukua huyu au kuona ni nani atakuwa Prime Minister ndiyo apelekwe kwa President hilo jambo atengeneze. Na vile nimesema ni mtu ambaye atafanya kazi kutoka kwa kazi yote ya nchi itakuwa juu yake lakini atakuwa anawasiliana na President hapo juu. Ndiyo nimesema President ni kama mtu yuko na zile powers ambazo ni ceremonial lakini day-to-day running of the government inafanywa na Prime Minister na cabinet.

Sasa Ministers kwa constitution hii, Minister ingawa anatoka nje ya bunge kukiwa na jambo kwa parliament ataitwa aende aulizwe, aelezee parliament jambo hili liko namna gani. Sasa kama strike ya waalimu iko saa hii, minister aende aambie bunge kitu gani kinaendelea na watatatua namna gani. Sasa kwa ufupi hiyo ndiyo kazi itafanywa na office ya President, atakuwa mtu ambaye amepigiwa kura na wananchi wote ambapo mtu atakuwa amepata kura tuseme akipata kura hamsini na moja kwa nchi yote, hamsini na moja 51% huyo ndiye ataenda kuwa President, na tena apate 20% kwa five provinces, lazima nafafanue hapo. Apate 20% kwa sababu kuna provinces nane hapa Kenya, lazima apate more than 50%, kwa hivyo atapata 20% of votes from five provinces halafu apate 51% kwa jumla, huyo ndiye atakuwa President wa Kenya. Hilo ndilo jambo ambalo lipo hapa.

Mambo mengine mnaweza kujisomea wenyewe, kwa appointment ya Prime Minister vile atafanya na term of office, wengine wamesema Prime Minister atakufia kwa ofisi akiwa ni Prime Minister lakini inalingana na vile chama ambacho kilimchukua

kuwa Prime Minsiter kitafanya kwa kura zingine. Lakini kikiendelea atakuwa hapo vile chama kinaendelea kuwa hapo na uwingi kwa parliament.

Sasa mambo ya dismissal, mambo ya mishahara, conduct of the cabinet na mambo mengine yako hapo sitaki kuwachosha nataka tu kufanya highlight ya yale mambo ambayo yanakuja kwa executive au kwa President, wakati huu unaokuja kwa hii constitution. Jambo kubwa ni ya kwamba sasa powers zile nyingi zimetoka, zile za kusema labda he is above law zimetoka. Ijapokuwa huyu ukiwa unataka kumpeleka kwa korti kutokana na private matter unaweza, private prosecution, lakini huwezi kumpeleka korti kama yeye yuko kwa kiti kwa jambo lingine lisilo private huwezi, hapo inasemeka hawezi na kweli kwa heshima ya nchi sio vizuri. Hiyo imemtetea sana, hatuwezi kusema tunapeleka President vile tunataka, kuna legislation hapa au constitution hii inasema lazima iwe kwa private capacity na lazima uchukue lengo fulani fulani ile ………..(Inaudible).

Sasa labda nitawachia hapo, kama kuna swali mnaweza kuja halafu.

**Stephen Muikuta:** …………………..(Inaudible) kumtajia mnyambuliko ……….(Inaudible) nafikiri jambo moja ningependa kuongeza ………….(Inaudible). Jina langu ni Stephen Muikuta…………….(Inaudible).
Kile tu ningeomba tulikuwa tunaona mara nyingi President ………………….(Inaudible) hata kama ni mambo ya ………….(Inaudible) ambayo inafanyika katika …………..(?) kusema ya kwamba………………(Inaudible). Halafu heshima zile ambazo zinapewa zote lazima …………….(Inaudible) kwamba mtu akiwa hana heshima sio vizuri labda kama ni kumpeleka korti ama ni baadaye mara amemaliza kazi yake anaweza kuwa amekufanyia kosa lakini wakati akiwa kiti tunaomba zile heshima zote apewe. Halafu ………..(Inaudible) Vice President ni yale yote President anaambiwa afanye alipochaguliwa …………………(Inaudible).

Mambo ya ministries ile wanasema kumi na tano, mimi napendekeza iwe na ………(Inaudible). Halafu term ya Minister najua hapa tunachagua mbunge na hata mbunge akiwa waziri labda sasa si itakuwa mbunge hatakuwa na faida katika parliament, bali mimi naonelea mbunge anapochaguliwa kama ako na zile qualities za kuwa minister pia aweze kupatiwa cheo. Wale wamechaguliwa na wananchi, halafu ikifika hapo ile mambo ya kura ambapo sasa…….(Inaudible) ile ………..(Inaudible) bonus katika polling stations you will be………………..(Inaudible).

**Maurice Ole Raria:** Umesema ya kwamba ungependelea kwamba Rais aweze kusema ya kwamba maendeleo fulani yafanyike katika district fulani sikuelewa vizuri. Wakati tutakuja kwa usambazaji wa mamlaka mtakuja kukubaliana na mimi ya kwamba hii haitawezekana. Ni kwa sababu kila tutakuwa na serikali za wilaya ama district councils na zitapatiwa nguvu za kutunga sheria hata tutakuwa nguvu hata ya kuandika wafanyikazi, district councils zitakuwa na serikali katika kiwango cha wilaya na kutakuwa na serikali katika kiwango cha location, na kutakuwa na serikali kwa kiwango cha kijiji. Kwa hivyo ni juu ya district council kuketi katika mabaraza yake na kuona ni sehemu gani katika hiyo wilaya inahitaji development ya aina fulani na itakuwa ni jukumu la district council kuona ya kwamba hili jambo ni muhimu kwa hivyo linapaswa kuzingatiwa. Kwa sababu

tukisema kwamba au wananchi walisema ya kwamba wanahitaji uongozi uende kwa mikono ya wananchi na tena hapa unapendekeza ya kwamba hayo mamlaka ya maendeleo yarudi tena kwa mikono ya Rais, basi itakuwa kama pengine unasema kama Rais atakuwa wa chama fulani na pengine katika wilaya yako nyinyi mko katika chama kingine basi kama huyo Rais hapendelei hicho chama ambacho kiko katika hiyo wilaya yako. Hakuna siku moja ataweza kuleta maendeleo katika wilaya yako na utakubaliana na mimi ya kwamba mambo ya Rais kuweza kupendelea ama serikali kuweza kupendelea sehemu zingine ni shida ambayo wananchi walisema inahitaji kuzingatiwa.

Na basi tunasema ya kwamba juu ya maendeleo ya kila wilaya ni jukumu la serikali ya wilaya kuweza kuzingatia mambo hayo ya maendeleo. Kwa hivyo maendeleo hayatakuwa hivyo kwa sababu serikali ya wilaya itaweza kuwa na nguvu ya kuchukua au kutoza ushuru na ku-collect taxes. Levies, kutakuwa na fedha kutoka kwa national resources ambazo zinapatikana katika sehemu zao na pia kutakuwa na district funds ambazo zitakuwa ziinaletwa kutoka national government. Kwa kila district kutakuwa na fedha ambazo zitatumwa pale, kwa hivyo hauna haja tena mtu mwingine kuja kusema pengine mnahitaji maendeleo fulani, mtakuwa mmpewa uongozi nyinyi wananchi wa wilaya ya Trans-Mara. Kwa hivyo sioni sababu yoyote ya nyinyi tena kwenda kutafuata nje ya wilaya kukiwa na human resource na mko na other resources, sioni sababu yoyote ya kutoka kwa mila yenu mtafute usaidizi wa kutoka nje.

Tumesema pia ni vyema na ni haki kwamba Rais wa nchi apewe heshima na katika Katiba hii tumesema kwamba Rais is the symbol of national unity, ni yeye ndiye anasimamia hatma ya nchi. Kwa hivyo Katiba hii inatambua ya kwamba lazima Rais awe anatambulika kwa sababu yeye ni symbol of national unity na ni jukumu la kila mwananchi kwa sababu atakuwa amepita na atakuwa anaungwa mikono na wananchi, basi ni jukumu la wananchi kuweza kuheshimu Rais wao kama kiongozi wa nchi yao.

Na pia Katiba hii imesema wakati ule Rais atakuwa katika mamlaka hakuna kesi yoyote mwananchi yeyote anapaswa kupeleka ama shirika lolote linaweza kwenda kushtaki Rais ikiwa angali katika hatamu, kwa sababu iwapo Rais atakuwa akishtakiwa mara kwa mara basi atashindwa kutekeleza jukumu zake za kuendesha taifa. Lakini inasemekana ya kwamba Katiba hii imesema hapa kama kosa ambalo Rais amefanya ni la kibinafsi nje ya ofisi tuseme Rais amefanya kitu kule nyumbani kwake, pengine amekosana na mfanyikazi wake na akampiga kofi, kwa mfano tu, basi huyo mtu anaweza kwenda kumshtaki kwa sababu hiyo hailingani na ofisi, hilo ni jambo la kibinafsi. Kwa hivyo wewe unaweza kupeleka kesi kama hiyo ya kibinafsi, unaweza kupeleka kortini. Lakini Katiba inamlinda Rais ili kulingana na mambo yoyote ambayo yamejulikana na majukumu ya Katiba, hauwezi kumshtaki wakati ako katika hatamu.

Lakini Katiba hii inasema kuna uwezekano kwamba wakati atamaliza hatamu yake ama wakati ata-retire ama akimaliza awamu yake kama kuna shida zozote kubwa ambazo amefanya kama pengine kuguza Katiba ama shida zingine kama za kuporomosha uchumi wa nchi, basi hapo anaweza kushtakiwa. Lakini tunasema kwa wakati huu, wakati huu wa mpito basi Rais aliye mamlakani wakati huu anahitajika katika Katiba apatiwe hatma, apatiwe heshima na apatiwe marupurupu yake yote na hakuna kesi yoyote au hawezi kushtakiwa kwa kesi aina yeyote kwa sababu Wakenya walipendelea wakati wa mpito ama transition

ambayo ni ya amani. Kwa hivyo wamesema kuwa Rais ambaye ako katika hatamu wakati huu, wakati atakapoondoka ofisini akienda katika mapumziko Katiba hii inamlinda kutokana na kesi zozote ambazo zinaweza, au hawezi kushtakiwa kwa sababu yoyote. Na kwamba atapata marupurupu yake yote vile will ama vitu ambavyo vilipitishiwa katika bunge inavyostahili.

Na pia tumezungumzia juu ya mambo ya mmeonelea kwamba ni vizuri kama Wabunge ambao mnawachagua waweze pia kuwa Mawaziri iwapo wako na qualifications zinazohitajika. Ningependa kukuhakikishia ya kwamba jambo hili lilizungumuziwa kwa kirefu sana katika mjadala wa commissioners na walisema ya kwamba, Wabunge ambao huwa wanachaguliwa na wananchi, wewe mwananchi huwa ukichagua Mbunge huwa haumchagui ili aende akuwe Waziri, huwa unamchaga ili aweze kutimiza malengo yenu na sio aende akuwe waziri. Kuwa Waziri ni jambo la ziada tu lakini juu ya yote ni kwamba kwanza atekeleze mambo katika constituency yake. Na pia kulikuwa na ulalamishi ya kwamba ikiwa Mbunge anakuwa Waziri na anatokomea, hakuji katika sehemu yake ya wakilishi bungeni na wakati mkimuuliza “Mjumbe mbona unapotea”? “Anasema wajua mimi ni Waziri na niko na kazi nyingi nimetumwa na Mzee hapa na pale”. Kwa hivyo anakuwa na kisababu cha kukosa kutimiza kazi ambayo nyinyi mmempatia, nyinyi mmemuandika kazi kwa kumchagua ili aweze kuwatumikia. Kwa hivyo tunasema hapo ndio au kisingizio chochote cha kuwacha watu waliowachagua wasiwe Mawaziri ili kazi yao haswa iwe ya kutumikia wananchi wa waliowachagua.

**George Nakholi:** Nikiongezea kitu kidogo hapo vile mtaambiwa tena na Bwana ole Raria wale Wajumbe mtawachagua kwa hii constitution mtakuwa na ile power ya recall yaani wasipofika kwa constituency na watu asilimia thelathini (30%) wanasema huyu Mjumbe hatumuoni hatufanyii kazi mnaweza kupata yeye kurudishwa ili elections zifanywe tena, hiyo iko kwa constitution yetu ya saa hii. Kwa hivyo ni vizuri yeye awe tu Member of Parliament awatumikie lakini watu wengine wafanye kazi ya administerial duties.

**Speaker:** …………………………..(Inaudible).

**George Nakholi:** Lakini sasa hiyo mambo nataka iwe hapa nchini.

**Maurice Ole Raria:** Kabla….

**George Nakholi:** Basi, wacha amalize, wacha amalize utaongea.

**Maurice Ole Raria:** Tutawapatia nafasi ya kuchangia katika mjadala huu lakini ningependa tu kumalizia hoja ambazo mmetoa na umesema ya kwamba wewe ungependelea kama baraza la mawaziri liwe ishirini na mbili. Na tume ilionelea na hayo yalikuwa ni maoni ya wananchi ya kwamba kuna wizara nyingi ambazo zimeweza kubuniwa kusudi ya kuwapa zawadi sehemu fulani ambazo ziliweza kuchagua pengine chama tawala na wala sio hasa kwa sababu ya kuendesha kazi za nchi. Unakuta kuna wizara zingine zimebuniwa ambazo kwa kusema kweli zingeweza kuunganishwa kwa wizara moja na ziweze kufanya kazi

sambamba. Kwa mfano kuna Social Services halafu kulikuwa na wakati ambapo Ministry ya Women Affairs iliundwa na hayo ni mambo ambayo yanaweza shughulikwa katika Ministry of Social Services kusudi tu kufuraisha akina mama. Mwerere Mwachai Mheshimiwa huyo akapatiwa hiyo wizara akaambiwa endesha hiyo wizara ili akina mama wafurahi, na alipoenda mbali akakuta hakuna kitu, na akasema sitaki wizara kwa hivyo hiyo wizara ikavunjwa.

Kwa hivyo wananchi walionelewa kuna nyakati nyingi kuna kubuni wizara bila kuzingatia haki ama haki ya kuendesha taifa. Hivyo basi wananchi walionelea kwamba ni lazima kuwe na wizara chache ambazo ziko na nguvu na ambazo hazifanyi kazi duplication of roles. Utakuta kuna wakati huu kuna wizara nyingi ambazo zinafanya kazi ambazo ni sawa ama kwa wizara moja unaweza kuta mawaziri kama watatu ambao hata hao wanagongana kwa sababu hawajui mipaka. Kwa hivyo tume ya Kurekebisha Katiba ilionelea ya kwamba ni vizuri kuwe na wizara chache ambazo ziko na nguvu na ili serikali isitumie pesa bure kuwa na wizara nyingi ambazo hata kazi zao hazionekani.

**Speaker:** Mimi ningependelea kwamba kwa sababu hiyo ni …………..(Inaudible) ambazo zinaweza kutokea wakati wa ziada …………………..(Inaudible), ijapokuwa tulikuwa tunalalamika ya kwamba pesa hakuna …………(Inaudible). Maneno hiyo yote ya President ……………………….(Inaudible). Hii maneno ya kusema 20% katika constituency, je kama mtu mmempenda mtu ama pengine inaweza kuwa ni Turkana, na hatujakuwa sisi Wakenya apate ile 51% na akose kwa hizi ishirini kwa sababu ni kabila mbovu, tunakupenda lakini hawezi kupata nje kutoka Nairobi, hawezi kwa Central. Naona mimi ni kwamba hivyo wazee ni wa kutoka province iweze kutolewa, mtu tu mradi apate 51% ya total vote ya Kenya.

Jambo lingine ni lazima, ni mtu ambaye ameoa na nataka ………..(Inaudible) vile aende mbele ya wananchi kwa sababu ni jamii anaongoza jamii ambayo iko na wanawake na wanajua hiyo shida sana, bibi yake aonekane awe first lady tumuone.

Jambo lingine mnajua Kenya hakukuwa na ………………….(Inaudible) na lazima President awe mtu ako na degree, isisemekane district fulani ama watu………(Inaudible) tunasikia watu wanaenda nje, devil worshipper kwanza yeye ni devil worshipper na ………..(Inaudible) ndio tuone, kila mtu hawezi.

Ukikuja kwa Prime Minister tunaona hayo ni ………….(Inaudible) yote yale………(?) mimi kwangu naona ile, basi siku moja tu ndio imebaki sisi ni wananchi na ikiwa mabadiliko kuna watu wengine walisema Wazungu wakienda hatutaweza kutawala. Yaani ………..(Inaudible) Mwafrika hawezi kutawala na lazima mabadiliko ………..(?) kulingana na maoni ya wananchi, kama ni maoni ya wabunge tu ndio mnaongea hivyo, mimi ningeona kwamba hiyo haina maana kwa sababu ni ………….(Inaudible). Lakini kwa sababu ya kati hao ndio inataka commission itoe ile ambayo hawataki…………..(Inaudible) wanafanya kwamba kiasi fulani ndio watoe hiy. Lazima moani hata kama inachoma kwa sababu ……………(Inaudible) kwa sababu waafrika walikuwa wanasema hati sisi DC hawezi kubali ya kwamba huo mshahara wake unaweza kuvunjwa na hata chifu hawezi kubali na hatakubali mpaka ifanyike. Kwa hivyo hata naye Prime Minister awe vivyo hivyo na masharti ni yale ya President.

**Maurice Ole Raria:** …………………………………………(inaudible) nataka kukuhakikishia ya kwamba katika report na idadi ya watu kuzungumzia juu ya ……………(Inaudible) itakuwa parliament, na evidence iko kwa police ambayo sisi, hiyo haiwezi…………(Inaudible) inaitwa evidence ama petition. Hii ni kuonyesha wananchi kwamba yale mambo ambayo Katiba imezingatia hapa sio mambo ya tume ya kubadilisha Katiba bali ni ya wananchi, hii ni kusema kwamba kama ni kusema ya kwamba Rais awe chini ya sheria muonyeshwe ni nani amesema hivyo. Mkisema kwamba ni Philemon Kibuku katika hearing ya Trans-Mara katika Hall fulani, tarehe fulani alisema juu ya Rais. Kwa hivyo hii itakuwa katika ………..(Inaudible) na wale wataenda katika National Conference mtaona ya kwamba haya maneno ambayo yameandikwa hapa ni maneno yenu pekee.

**George Nakholi:** …………………..(Inaudible).

**Maurice Ole Raria**……………………………………………..(Inaudible) kwa hivyo pia tunawahakikishia kwamba yameandikwa katika ofisi, hiyo ofisi ni yenu na ni ya wananchi, kwa hivyo mnaweza kwenda CKRC …………………..(Inaudible) na mkienda katika data analysis department mtaenda ………………………..(Inaudible) mkijua ni ni …………..(Inaudible) walisema juu ya provincial administration ……………..(Inaudible) kuhakikisha……….(Inaudible) namna hii nituwaletea ripoti nzima ya taifa. Sio kusema kwamba ni rahisi kwa sababu hili ni jambo ambalo …………….(Inaudible) wananchi na hasa kwa sababu memorandums nyingi zilikuwa ………….(Inaudible) na walisema ya kwamba ………..(Inaudible) Rais wa nchi awe ……….(Inaudible) fulani, kwa hivyo tunaona kama …………….(Inaudible) ni lazima ………………………(Inaudible).

Pia ulisema ya kwamba lazima Rais awe na degree na ningetaka kuwaambia ya kwamba sifikiri kwamba Rais anayekuwa………………(Inaudible) kwa sababu yeye ni………..(?) na kama ni mama awe na mzee. Kwa hivyo hiyo ni kati ya moral na zile zilikuwa zinaitwa moral, mkasema …………..(Inaudible) one of the qualification the………………….(Inaudible) ni morally upright. Na nikiongea juu ya kuwa morally upright mambo kama hizo za marriage.

Actually wananchi walisema the President should be married and he should not just be married but should be married, live together with the wife or the husband and happily married. Kuwa isiwe Rais ameoa lakini hayuko na watoto wake………(Inaudible). Kwa hivyo wananchi mtaona kwa hiyo report……………..(Inaudible) wanahitaji yule Rais ambaye ameoa ama ameolewa na anaishi na bwana au bibi yake.

Na pia mmezungumzia juu ya mambo ya percentage kwamba votes zile inahitajika kama mgombea wa urais anaweza pata asilimia ya kura hamsini na moja basi………………(Inaudible) katika …………..(Inaudible) and of course. Na ningependa kukuambia ya kwamba ni hatari kusema hivyo kwa sababu Katiba ………….(Inaudible). Hili pendekezo la 20 per cent katika kila mkoa hii ni kuhakikisha ya kwamba Rais ………………………..(Inaudible) kwa sababu mtakubaliana na mimi ya

kwamba kuna jamii, ama kuna makabila katika nchi yetu ambao wao wenyewe wanaweza kutaka asilimia hamsini na moja kutoka mkoa moja, mnakubaliana na mimi? Inawezekana, kwa hivyo hiyo sababu ya ………………..(Inaudible) awe amefanya…………..(Inaudible) kwa sababu tukisema tukiwapa 51% basi tuna uhakika wewe ukiwa Maasai siku mmoja hautaongoza. Kwa hivyo ………….(Inaudible) sababu ya kuwa na hiyo …………………………(Inaudible).

**Speaker:** ……………………………………………(Inaudible)

**NOTE:** Tape four and five were completely inaudible and therefore this report is incomplete.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**